# Kiswahili

## 1

Kitabu cha Mwanafunzi



**Tusome Early Literacy Programme**

# Yaliyomo

Utangulizi ........................................ ii
Dibaji ........................................ ii
Wiki ya 1 ........................................ 1
Wiki ya 2 ........................................ 6
Wiki ya 3 ........................................ 11
Wiki ya 4 ........................................ 16
Wiki ya 5 ........................................ 21
Wiki ya 6 ........................................ 26
Wiki ya 7 ........................................ 31
Wiki ya 8 ........................................ 36
Wiki ya 9 ........................................ 41
Wiki ya 10 ........................................ 46
Wiki ya 11 ........................................ 51
Wiki ya 12 ........................................ 56
Wiki ya 13 ........................................ 61
Wiki ya 14 ........................................ 66
Wiki ya 15 ........................................ 71
Wiki ya 16 ........................................ 76
Wiki ya 17 ........................................ 81
Wiki ya 18 ........................................ 86
Wiki ya 19 ........................................ 91
Wiki ya 20 ........................................ 96
Wiki ya 21 ........................................ 101
Wiki ya 22 ........................................ 106
Wiki ya 23 ........................................ 111
Wiki ya 24 ........................................ 116
Wiki ya 25 ........................................ 121
Wiki ya 26 ........................................ 126
Wiki ya 27 ........................................ 131
Wiki ya 28 ........................................ 136
Wiki ya 29 ........................................ 141
Wiki ya 30 ........................................ 146

## Utangulizi

Tangu kupata uhuru, serikali ya Kenya imetambua elimu kama mojawapo ya haki za kimsingi za binadamu; kwa hivyo imejitolea kuwapa wananchi wake wote elimu bora. Raslimali nyingi zimewekezwa ili kuimarisha upatikanaji, umuhimu, usawa na ubora, vipengee ambavyo vimeboresha miundomsingi na kuongeza idadi ya wanaohudhuria masomo katika nyanja tofauti za elimu na mafundisho.

Serikali inatambua ya kwamba ili kuweza kushindana katika nyanja za kimataifa na kuimarika kiuchumi, taifa linahitaji elimu inayowawezesha wananchi kuwa wabunifu, kupata elimu ya kudumu maishani na wanaoweza kufanya kazi zilizo tata na zenye changamoto. Elimu pia inafaa kuwawezesha wananchi kutatua shida katika jamii, kukata shauri, kufanya kazi bila kufuatiliwa, kuwajibika na pia waweze kusoma, kupiga mambomsasa na kupata ujuzi wa kujidhihirisha. Maendeleo ya kudumu yanahitaji kila binadamu apate maarifa ya karne ya 21, ujuzi, mtazamo na maadili yanayohitajika kudumisha maisha ya siku za usoni. Mkazo unatiliwa kwenye elimu inayowezesha kusoma na kufanya hesabu. Nchi ya Kenya imefanya maendeleo katika kuhakikisha ubora wa elimu. Miradi mbalimbali imewekwa ili kuangazia ubora wa elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi.

Kitabu hiki cha Tusome, bila shaka, kitaimarisha masomo kuanzia darasa la 1 na la 2 ya shule za msingi kwenye somo la kujua kusoma na kuandika. Mpangilio wa masomo unahakikisha ya kwamba wanafunzi wote nchini Kenya wanaweza kusoma na kuelewa ifikapo mwisho wa mwaka. Kwa hivyo, nawahimiza washirika wetu waendelee kusaidia sekta ya elimu katika utekelezaji wa mikakati na mbinu ili kuboresha elimu.

**Prof. Jacob T. Kaimenyi**, PhD, FICD, EBS

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

## Dibaji

Lengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote bila kuzingatia hali yao ya kuichumi na kijamii. Mabadiliko yamefanywa ili kuimarisha sekta ya elimu. Mabadiliko haya yana mtazamo wa kuifanya nchi ishindane kimataifa. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa na Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki mwa Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) inaonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuboresha mafanikio katika uwezo wa kusoma na kufanya hesabu.

Maendeleo yaliyofanyika hivi karibuni katika nchi ya Kenya yalionyesha kuwa kuna haja zaidi ya kuwa na mfumo wenye kina wa kuhakikisha ubora wa elimu. Mabadiliko haya yamo katika Katiba ya Kenya (2010) na Ruwaza ya Kenya ya 2030. Katiba ya Kenya inahakikishia kila mtoto nchini masomo ya msingi yasiyo na malipo. Vilevile, Ruwaza ya Kenya ya 2030 inatarajia kuhakikisha kuwa kuna mabadiliko ya kimaendeleo nchini na pia ushindani katika nyanja za kimataifa ifikapo mwaka wa 2030. Kati ya matarajio ni kutoa elimu bora na mafundisho ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi wa hali ya juu. Mfumo uwe wa kupatia wanafunzi ujuzi wa kazi utakaounganisha nchi na soko la kimataifa. Nakala ya Kikao Cha Bunge Nambari 14 ya 2012 inaonyesha njia mwafaka na wanafunzi asilimia mia moja waweze kukamilisha masomo katika elimu ya msingi bila kuathiri ubora wa elimu.

Wizara ya elimu inatazamia kuboresha elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi hasa ikizingatia uwezo wa kusoma na kuandika na kufanya hesabu. Mradi wa Kitaifa wa Tusome unaodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika (USAID) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), unakusudia kuboresha matokeo ya kuweza kusoma na kuandika katika madarasa ya 1 na ya 2. Mradi huu unalenga kuboresha uwezo wa walimu wa kuelekeza darasani, kuhakikisha wanafunzi wamepata vitabu sahihi vya kusoma na vya ziada, na kuwaelekeza walimu kupitia kwa wakufunzi wa mashauri ya walimu (TAC Tutors) na walimu wakuu. Halikadhalika, utaanzisha njia mwafaka za kufuatilia na kutathmini matokeo ambayo itaunganisha mafunzo na matokeo katika kujifunza kusoma na kuandika. Mradi huu utatumia teknolojia ili kuimarisha mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na kuongeza uwezo wa sekta ya elimu kuboresha matokeo ya masomo.

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu, ninawasihi washikadau wote kushirikiana ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Tusome umefua dafu.

**Dkt. Belio R. Kipsang**

Katibu Mkuu,

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia: Idara ya Elimu




Tamka sauti.

**m**

Soma neno.

**anaona** **paka** **mama**

## Koki na Mugambi

Kuna marafiki wawili. Msichana anaitwa Koki na mvulana anaitwa Mugambi.  Koki na Mugambi huenda  kila asubuhi na mapema. Njiani, wao huona vitu mbalimbali. Koki anaona . Mugambi anaona . Koki anaona . Mugambi anaona . Wanapofika shule, Koki na Mugambi wanaona majengo ya shule. Koki anaona . Mugambi anaona . Koki na Mugambi wanaona .

Tamka sauti.

**M** **m**

Soma neno.


**anaona** **paka** **mama**


## Koki na Mugambi

Baada ya masomo, Koki na Mugambi hurudi  .

Wakiwa nyumbani, Mugambi anaona 

na  . Koki anaona 

na  . Mugambi anaona  na

 . Wote wanaona  .

Tamka sauti.

■ **a** **m**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● m a a

**ma** **a**

Soma silabi na maneno.

▬ ma ma a ma

**mama** **ama**

Tamka sauti.

▲ **A** **a**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ m a a m aa

**ma** **a** **maa**

Soma silabi na maneno.

★ ma ma a ma

**mama** **ama**



## Mama na Paka

Mama anaona paka.

Paka anaona mama.

Tamka sauti.

■ **m M** **a A**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

★ m a a

**ma** **a**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano a ma - **ama**.

●

| | | | |
|---|---|---|---|
| **ma** | **a** | **ma** | **a** |

## Katumbo



Tamka sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ■ | **u** | **a** | **m** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ● | u | m u | a | m a |
| | **u** | **mu** | **a** | **ma** |

Soma silabi na maneno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▬ | ma ma | ma u a | u a | u ma |
| | **mama** | **maua** | **ua** | **uma** |

Tamka sauti.

| | | |
|---|---|---|
| ▲ | **U** | **u** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ⬬ | u u | mu u | a a | ma a |
| | **uu** | **muu** | **aa** | **maa** |

Soma neno zima.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ★ | **anaona** | **paka** | **na** |



## Paka na Ua

Mama anaona uma na maua.

Paka anaona ua.

Paka uma ua.

Tamka sauti.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ■ | **k** | **m** | **a** | **u** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ● | k a | k u | ka a | ku u |
| | **ka** | **ku** | **kaa** | **kuu** |

Soma silabi na maneno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▬ | ku ku | u ku ta | ka ka | a mu a |
| | **kuku** | **ukuta** | **kaka** | **amua** |

Tamka sauti.

| | | |
|---|---|---|
| ▲ | **K** | **k** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ⬬ | k a | k u | m a | m u |
| | **ka** | **ku** | **ma** | **mu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ★ | a ka amua | a ka mu uma |
| | **akaamua** | **akamuuma** |
| | ku kaa | |
| | **kukaa** | |



## Paka na Kaka

Paka akaamua kukaa.

Mama akaamua kukaa.

Kaka akaamua kukaa.

Paka akamuuma kaka.

Paka akamuuma mama.

Tamka sauti.

■ u U k K

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: ma ka a – **makaa**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma | ka | u | ka |
| kaa | mu | k | a |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● Paka **na** uma.
Uma **na** makaa.
Mama **na** kaa.
Kaka **na** mama.

## Mama na Paka



Mama anaona paka na ua.

Kaka anaona uma na makaa.

Paka anaona mama na kaa.

Kaka akaamua kukaa na paka.

Tamka sauti.

t k u

Tamka sauti ya herufi na silabi.

t a ta a t u tu u

**ta** **taa** **tu** **tuu**

Soma silabi na maneno.

ta ka ta ka a ta ka

**takataka** **ataka**

a ka ta ka a mu

**akataka** **amu**

Tamka sauti.

T t

Tamka sauti ya herufi na silabi.

tu u ku u mu u k u

**tuu** **kuu** **muu** **ku**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku mu ua a ka taka

**kumuua** **akataka**

ku mu uma a ka kataa

**kumuuma** **akakataa**



## Kaka na Amu

Kaka anaona takataka.

Mama anaona takataka na makaa.

Amu anaona takataka, makaa na kaa.

Kaa akataka kumuuma amu.

Amu akakataa kumuua kaa.

Tamka sauti.

■ **l** **t** **k**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● t i m i k i i

**ti** **mi** **ki** **i**

Soma silabi na maneno.

▬ ti ki ti ki ma m ku u ma ka a

**tikiti** **kima** **mkuu** **makaa**

Tamka sauti.

▲ **l** **i**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ ti i mi i ki i i i

**tii** **mii** **kii** **ii**


Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a ka kaa a ka taka

**akakaa** **akataka**

a ka ka taa ku kaa

**akakataa** **kukaa**



## Mama na Kima Mkuu

Mama anaona Kima mkuu.

Kima mkuu anaona mama.

Mama anaona tikiti na uki mtamu.

Kima mkuu akataka kukaa na mama na amu.

Amu akakataa kukaa na kima mkuu na mama.

Mama akakataa kukaa na amu.

Mama akakaa na kima mkuu.

Tamka sauti.

■ t T i I

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno. Kwa mfano: ta tu - **tatu**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| **ma** | **mi** | **mu** | **ta** |
| **tu** | **ki** | **ku** | **ka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| **Wakati uliopo** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Mama **ana**kaa | Mama **ata**kaa. |
| Mama **ana**taka | Mama **ata**taka. |
| Mama **ana**kataa | Mama **ata**kataa. |



## Amu na Matatu

Amu ataka matatu kuukuu na taa.
Kaka ataka takataka na makaa.
Kama amu atataka takataka na makaa, kaka atakataa katakata.

Tamka sauti.

n i t

Soma sauti ya herufi na silabi.

n a n u n i t u

**na** **nu** **ni** **tu**

Soma silabi na maneno.

m ti ni ki ti ni a na ka a a na o na

**mtini** **kitini** **anakaa** **anaona**

Tamka sauti.

N n

Tamka sauti ya herufi na silabi.

n a k a m a t a

**na** **ka** **ma** **ta**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a na taka
**anataka**

a na ona
**anaona**

a na kataa
**anakataa**

a na tamani
**anatamani**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mkate unanukia | Mikate inanukia. |
| Mti unanukia | Miti inanukia. |



## Tai Mkuu

Tai mkuu anakaa mtini.

Paka anakaa na kuku kitini.

Tai mkuu anaona paka na kuku.

Tai mkuu anataka kukaa na kuku.

Paka anakataa.

Tai mkuu anatamani kukaa na paka.

Kuku anakataa.

Tai mkuu ana...

Tamka sauti.

**o** **n** **i**

Soma sauti ya herufi na silabi.

n o k o m o t o

**no** **ko** **mo** **to**

Soma silabi na maneno.

no no mo to mo to ni m to to

**nono** **moto** **motoni** **mtoto**

Tamka sauti.

**O** **o**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

n o n oo n i n ii

**no** **noo** **ni** **nii**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a na taka a na toa

**anataka** **anatoa**

a na ota a na kata

**anaota** **anakata**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| kaa | **ma**kaa |
| ini | **ma**ini |
| tikiti | **ma**tikiti |



## Kanini na Katana

Kanini ni mtoto.

Anakaa na kaka Katana.

Katana anakata kuni. Kanini anaota moto.

Motoni mna ini nono.

Katana anaona konokono.

Anatoa mkuki. Anataka kuua konokono.

Katana anataka kutia konokono motoni.

Kanini anakataa.

Tamka sauti.

■ **n N** **o O**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno. Kwa mfano: mo to - **moto**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | na | mo | i | kaa | ni |
| a | to | ta | ka | u | no |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Wakati uliopo (sasa) | Wakati ujao (kesho) |
|---|---|
| Koki **ana**lia | Koki **ata**lia. |
| Kamau **ana**nunua | Kamau **ata**nunua. |
| Koki **ana**tamani | Koki **ata**tamani. |
| Kamau **ana**mkatia | Kamau **ata**mkatia. |

## Kamau na Koki

Kamau ananunua kaimati,
asali na maini.
Koki anatamani asali.

Kamau anakataa kumpatia.

Koki anataka maini.
Kamau anakataa kumkatia.

Koki analia,

"Kamau nataka kaimati."
Kamau anamkatia kaimati.

Kaimati ni tamu.



Tamka sauti.

**w** **o** **n**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a w i w u w o

**wa** **wi** **wu** **wo**

Soma silabi na maneno.

wa tu wa to to wa na wa ta no

**watu** **watoto** **wana** **watano**

Tamka sauti.

**W** **w**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

w a k o n a t o

**wa** **ko** **na** **to**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka taka wa ka wa toa


**wakataka** **wakawatoa**

a ka wa ona a ka wa ita

**akawaona** **akawaita**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mama **a**kamwona mtu | Mama **wa**kawaona watu. |
| Mama **a**kamtoa kuku | Mama **wa**kawatoa kuku. |
| Mama **a**kamwita mtoto | Mama **wa**kawaita watoto. |



## Watoto wa Kima

Kima ana watoto watano.

Watoto wa kima wana mikia mirefu.

Watoto wanataka mtama mtamu wa mama.

Mama anawaona watoto wa kima mtamani.

Mama anawaita watu.

Watu wanawatoa watoto wa kima mtamani.

Ungetaka kuwaona watoto wa kima wenye mikia mirefu?

Tamka sauti.

■ **e** **w** **o**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● n e t e w e m we

**ne** **te** **we** **mwe**

Soma silabi na maneno.

▬ te na Ne e ma m ke ka ni ma we

**tena** **Neema** **mkekani** **mawe**

Tamka sauti.

▲ **E** **e**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ w e k e w i w o

**we** **ke** **wi** **wo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a ka muona a ka muita

**akamuona** **akamuita**

a ka m timua a ki m kamata

**akamtimua** **akimkamata**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mtoto **a**nataka | Watoto **wa**nataka. |
| Mtoto **a**naona | Watoto **wa**naona. |
| Mtoto **a**natamani | Watoto **wa**natamani. |
| Mtoto **a**naokota | Watoto **wa**naokota. |



## Neema na Mwewe

Amina akaketi mkekani akiota moto.

Akamuona mwewe akimkamata kuku.

Akamuita Neema, “Neema, Neema!”

Neema akaitika, “Naam, Amina.”

Amina akaita tena, “Neema! Ona mwewe.”

Neema akaokota mawe na kumtimua mwewe.

Mwewe akatua mtini.

Amina na Neema wakaketi mkekani wakiota moto na kukata mkate.

Tamka sauti.

e E w W

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: wa tu - **watu**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ka | tu | m | wa | te | we |
| i | a | to | ma | mi | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

Wewe **una**taka - Mtoto **ana**taka.
Wewe **una**ona - Mtoto **ana**ona.
Wewe **una**ita - Mtoto **ana**ita.
Wewe **una**okota - Mtoto **ana**okota.

## Tai na mtoto wa paka



Owino ana watoto watatu: Wata, Wakio na Waki.
Watoto wa Owino wana mtoto wa paka.
Tai mtini anamuona mtoto wa paka.
Anatamani kumkamata mtoto wa paka.
Watoto wanaita Owino.
Owino anamuona tai na mtoto wa paka.
Owino anaokota tawi.

Tamka sauti.

■ l e w

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● l e l i l u l o

**le** **li** **lu** **lo**

Soma silabi na maneno.

▬ Lo la ni li ma u Ne li ma la ki ni

**Lolani** **limau** **Nelima** **lakini**

Tamka sauti.

▲ L l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ l a w e n e k e

**la** **we** **ne** **ke**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a ka m letea a ka litema

**akamletea** **akalitema**


a ki li tema li li kuwa

**akilitema** **lilikuwa**

Sarufi: Soma maneno haya.

◆

| Wakati uliopita | Wakati ujao |
|---|---|
| **ali**ona | **ata**ona |
| **ali**lala | **ata**lala |
| **ali**lia | **ata**lia |
| **ali**tamani | **ata**tamani |
| **ali**waletea | **ata**waletea |



## Lolani na Nelima

Lolani alilala kitini.

Nelima akamletea limau.

Lolani akala.

Lo! Limau lilikuwa kali.

Lolani akalitema limau na kulia.

Nelima akaona Lolani akilitema limau.

Nelima akamletea Lolani muwa.

Lakini Lolani hakula muwa.

Nelima akamletea asali.

Lolani akala asali.

Asali ni tamu.

Tamka sauti.

■ **h** **l** **e**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● h a h o h u h e

**ha** **ho** **hu** **he**

Soma silabi na maneno.

▬ ha mu ka ha wa ho te li ni He le na

**hamu** **kahawa** **hotelini** **Helena**

Tamka sauti.

▲ **H** **h**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ h i w i l i k i

**hi** **wi** **li** **ki**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a li nunua a ka m letea

**alinunua** **akamletea**

a ka tokea ha ku taka

**akatokea** **hakutaka**

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

◆
1. mama **mfupi**
2. mtoto **mrefu**
3. amu **mnene**
4. paka **mkubwa**



## Hotelini

Helena alinunua kaimati, mkate na kahawa hotelini.

Alikuwa na hamu ya kahawa tamu.

Mama akatokea na kuketi kitini.

Helena akamletea kahawa tamu, kaimati na mkate.

Lakini mama alitaka kula wali kwa maini.

Hakutaka kahawa tamu, kaimati na mkate kama Helena.

Tamka sauti.

■ **h H** **l L**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **hoteli**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| te | ho | ta | la | li | na |
| te | we | ti | ma | ni | le |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **akam**letea | **wakawa**letea |
| **aka**muona | **wakawa**ona |
| **aka**muita | **wakawa**ita |
| **aka**lia | **waka**lia |

## Halake na Lina



**Halake:** Niliokota lulu. Nikaiweka katika taulo.

**Lina:** Niliona taulo kitini. Nikaitoa na kuiweka uani. Niliona lulu na kuiokota.

**Halake:** (*Akimwambia Ali*) Nimemwona Lina na ile lulu.

**Ali:** Ninaitaka lulu. (*Lina anakataa*)

**Halake:** (*Akilia*) Mama! Mama!

**Lina:** Nimeiweka lulu kitini.

**Ali:** Lina ameiweka lulu kitini. *(Halake anaiokota ile lulu.)*

Tamka sauti.

s h l

Tamka sauti ya herufi na silabi.

s a s i s o s e

**sa** **si** **so** **se**

Soma silabi na maneno.

Sa u mu so ko a su bu hi Sa ra

**Saumu** **soko** **asubuhi** **Sara**

Tamka sauti.

**S** **s**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

s u h u l u w u

**su** **hu** **lu** **wu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li kutana

**walikutana**

wa li wa tesa

**waliwatesa**

ni ta wa sema

**nitawasema**

a li sononeka

**alisononeka**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **ali**watesa | **wali**watesa |
| **ali**wasema | **wali**wasema |
| **ali**kutana | **wali**kutana |
| **ali**sononeka | **wali**sononeka |



## Sara na Saumu

Sara na Saumu wanakaa Masii karibu na soko la Sokomoko.

Asubuhi walikutana na watoto sita wa mtaani.

Watoto hawa waliwatesa na kuwatusi Sara na Saumu.

Saumu alisononeka sana. Sara alikuwa na wasiwasi sana.

Sara akasema, “Msinitese wala kunitusi. Nitawasema kwa baba na mama.”

Wale watoto wakatoroka.

Tamka sauti.

**b** **s** **h**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

b a b e b u b o

**ba** **be** **bu** **bo**

Soma silabi na maneno.

bi s ku ti ba ku li bi ri ka m ke be

**biskuti** **bakuli** **birika** **mkebe**

Tamka sauti.

**B** **b**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

b i s i k i h i

**bi** **si** **ki** **hi**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li amka wa ka tamani

**waliamka** **wakatamani**

wa ka toa wa ka tabasamu

**wakatoa** **wakatabasamu**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mtoto **ali**amka | Watoto **wali**amka. |
| Mtoto **ali**toa | Watoto **wali**toa |
| Mtoto **ali**tamani | Watoto **wali**tamani. |
| Mtoto **ali**tabasamu | Watoto **wali**tabasamu. |



## Biskuti

Asubuhi baba, mama na watoto waliamka.

Watoto wakatamani kula biskuti.

Kulikuwa na bakuli, birika, bilauri na mkebe kabatini.

Mama akatoa birika akaona bilauri.

Watoto wakatoa bilauri wakaona buibui.

Baba, akamtoa buibui.

Watoto wakatoa mkebe, wakaona biskuti.

Watoto wakatabasamu.

Tamka sauti.

■ b B s S

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: u si ku - **usiku**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | ku | u | sa | ki | ba |
| si | li | na | bu | i | ha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mtu **aka**m**u**ona kuku | Watu **wa**ka**wa**ona kuku. |
| Mtu **aka**m**k**amata kuku | Watu **wa**ka**wa**kamata kuku. |
| Mtoto **a**ka**mu**ona buibui | Watoto **wa**ka**wa**ona buibui. |

## Wasia wa babu

Babu: Njooni hapa. Sikieni wasia huu. Nawasihi msome. Masomo ni muhimu sana. Masomo huleta hekima. Hekima huleta mali.



Watoto: Naam Babu. Sisi sote tutasoma.Usiwe na wasiwasi.

Babu: Msisahau kuwasiliana na walimu wenu.

Watoto: Naam Babu. Hatutasahau. Asante kwa wasia wako.

Tamka sauti.

■ **y** **b** **s**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● y a y e y i y u

**ya** **ye** **yi** **yu**

Soma silabi na maneno.

▬ ma ya i Ye ru sa he ka ya ya ya

**mayai** **Yerusa** **hekaya** **yaya**

Tamka sauti.

▲ **Y** **y**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ y o b o l o h o

**yo** **bo** **lo** **ho**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ hu tu okea hu tu somea

**hutuokea** **hutusomea**


a na ye tii a ta ku somea

**anayetii** **atakusomea**

Sarufi: Soma sentensi zifuatazo.

◆

| Huyu | Yule |
|---|---|
| 1. Yaya **huyu** ni mzuri | Yaya **yule** ni mzuri. |
| 2. Babu **huyu** ni mrefu | Babu **yule** ni mrefu. |
| 3. Paka **huyu** ni mkali | Paka **yule** ni mkali. |
| 4. Kuku **huyu** ni mnono | Kuku **yule** ni mnono. |



## Yerusa yaya wetu

Yaya wetu ni Yerusa.

Kila asubuhi Yerusa hutuokea keki na mayai.

Kabla ya kulala, yeye hutusomea hekaya tamu tamu.

Ukiwa mtoto mtiifu, Yerusa hukusomea hekaya nyingi wakati wa kulala. Hekaya huwa tamu.

Tamka sauti.

■ **z** **y** **b**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● z a z i z u z e

**za** **zi** **zu** **ze**

Soma silabi na maneno.

▬ zi zi ni za bi bu zi wa ni wa za zi

**zizini** **zabibu** **ziwani** **wazazi**

Tamka sauti.

▲ **Z** **z**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ z o s o y o b o

**zo** **so** **yo** **bo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ wa li elekea

**walielekea**

wa li kula

**walikula**

ku wa bebea

**kuwabebea**

wa ka wa nunulia

**wakawanunulia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Huu ni **m**nazi wetu | Hii ni **mi**nazi yetu. |
| Huu ni **m**zabibu wetu | Hii ni **mi**zabibu yetu. |
| Huu ni **m**limau wetu | Hii ni **mi**limau yetu. |
| Huu ni **m**mea wetu | Hii ni **mi**mea yetu. |
| Huu ni **m**kebe wetu | Hii ni **mi**kebe yetu. |



## Zani na Ziki

Ilikuwa wakati wa likizo. Zani na Ziki walikuwa na zamu ya kutazama zizi lao na ziwa.

Kila asubuhi walielekea zizini.

Baadaye walielekea ziwani.

Huko waliona minazi na mizabibu.

Walikula zabibu. Waliwabebea wazazi wao zabibu na nazi.

Wazazi wakawanunulia zawadi. Zani akanunuliwa zawadi ya zeze. Ziki akanunuliwa zawadi ya miwani.

Tamka sauti.

■ z Z y Y

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: wa za zi - **wazazi**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| si | ka | za | wa | wa | na |
| zi | ha | i | ma | ti | ki |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| 1. **an**akaa | **ali**kaa |
| 2. **an**aona | **ali**ona |
| 3. **an**alia | **ali**lia |
| 4. **an**ataka | **ali**taka |

## Ayoo

Ayoo ni mtoto. Baba yake ni Otieno. Mama yake anaitwa Kanini.



Yeye hukaa na babu yake wilayani Kikuyu. Kila siku Ayoo huletewa mayai na shangazi yake Zainabu.

Bibi humwekea mabuyu kibuyuni. Ayoo hutamani chakula kitamu zaidi ya mabuyu. Yeye huomba ili babu yake awe na mali.

Tamka sauti.

■ **g** **z** **y**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● g a g aa g e g i

**ga** **gaa** **ge** **gi**

Soma silabi na maneno.

▬ ki so go mi zi go ma go ti gaa gaa

**kisogo** **mizigo** **magoti** **gaagaa**

Tamka sauti.

▲ **G** **g**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ g u g i g o g oo

**gu** **gi** **go** **goo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ wa ka wa samehe wa ka watega

**wakawasamehe** **wakawatega**


wa ka wa ona wa ka gaagaa

**wakawaona** **wakagaagaa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hili ni bega | Haya ni **ma**bega. |
| Hili ni goti | Haya ni **ma**goti. |
| Hili ni sikio | Haya ni **ma**sikio. |
| Hili ni gego | Haya ni **ma**gego. |



## Wezi sokoni

Katika soko la Mogotio, kulitokea wezi watatu.
Walitaka kuiba mizigo sokoni.
Watu wakawaona.
Wezi wakataka kutoroka.
Watu wakawatega.
Mtego ukawakamata.
Wezi wakaumia sana.
Kuna wale waliumia visogo. Wengine wakaumia mabega, magoti na miguu.
Wezi wakagaagaa.
Muuguzi akawatibu.
Watu wakawasamehe.
Kutoka siku hiyo wezi hawakuiba tena.

Tamka sauti.

■ **d** **g** **z**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● d e d i d u d o

**de** **di** **du** **do**

Soma silabi na maneno.

▬ de be do li A di di da ki ka

**debe** **doli** **Adidi** **dakika**

Tamka sauti.

▲ **D** **d**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ d a b a d e b e

**da** **ba** **de** **be**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ wa ka elekea ku ni nunulia

**wakaelekea** **kuninunulia**

tu ta nunua a ka kubali

**tutanunua** **akakubali**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Hili** ni debe | **Haya** ni **ma**debe. |
| **Hili** ni godoro | **Haya** ni **ma**godoro. |
| **Hili** ni doli | **Haya** ni **ma**doli. |
| **Hili** ni dau | **Haya** ni **ma**dau. |



## Adidi na Baba sokoni

Baba aliita, “Adidi! Amka! Leo ni siku ya soko.”

Adidi aliamka baada ya dakika kumi.

Wakaelekea soko la Gede.

Baba akasema, “Adidi, leo tutanunua dagaa, dania, debe na godoro.”

Adidi akauliza, “Baba, unaweza kuninunulia soda, doli na gololi?”

“Sawa Adidi, nitakununulia.” Baba akakubali.

Tamka sauti.

■ g G d D

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: da ki ka - **dakika**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | go | ge | be | de | ki |
| da | ma | ti | ka | te | mu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

1. Kaka ali**enda** shuleni.
2. Mtoto ali**lia** kitini.
3. Jitu lili**simama** njiani.
4. Bibi ali**beba** mzigo.

## Kazi ya Kogo na Radoli

Kogo na Radoli walikaa Migori. Kazi yao ilikuwa kubeba mizigo mizito. Kila asubuhi walibeba magunia mazito ya mboga na mihogo. Kila usiku mabega na miguu yao iliuma sana. Walikula ugali kwa uyoga. Walikubaliana kugawana hela baada ya kazi.



Tamka sauti.

■ j d g

Tamka sauti.

● j a j aa j e j i

**ja** **jaa** **je** **ji**

Soma sentensi hizi.

1. Kaka alienda shuleni.
2. Mtoto alilia kitini.
3. Jitu lilisimama njiani.
4. Bibi alibeba mzigo.

Tamka sauti.

▲ J j

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ j u g u d u j o

**ju** **gu** **du** **jo**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ wa na kijiji wa ka mu amini

**wanakijiji** **wakamuamini**

ha wa ku amini a ka li patia

**hawakuamini** **akalipatia**


Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. Dada ameketi wapi?
2. Paka amesimama wapi?
3. Mwalimu ameandika wapi?
4. Jiwe liko wapi?









## Jilo na Jitu

Siku ya Jumatatu jioni, Jilo aliona jitu kijijini.

Akasema, “Nimeliona jitu majanini.” Wanakijiji hawakuamini.

Siku ya Jumanne, Jumatano na Alhamisi mchana akaliona jitu tena.



Siku ya Ijumaa asubuhi jitu likasema, “Jilo, nataka kula.”

Jilo alijawa na wasiwasi.

Akalipatia jitu jiwe la moto.

Jitu likala jiwe na kuzimia.

Siku ya Jumamosi walilizika jitu. Jumapili ilipofika walifanya sherehe kwa heshima ya Jilo. Wanakijiji wote walimwamini jilo.

Tamka sauti.

■ **r** **g** **j**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● r e r a r i r o

**re** **ra** **ri** **ro**

Soma silabi na maneno.

▬ ra i s ga ri ra di Ja nu a ri

**rais** **gari** **radi** **Januari**

Tamka sauti.

▲ **R** **r**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ r u j i w a g a

**ru** **ji** **wa** **ga**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ li li simama tu ka sikia

**lilisimama** **tukasikia**

a ki malizia wa ka torokea

**akimalizia** **wakatorokea**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Wakati uliopo** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Rais a**na**kuja kijijini | Rais a**ta**kuja kijijini. |
| Rais a**na**simama barabarani | Rais a**ta**simama barabarani. |
| Rais a**na**wasihi watu | Rais a**ta**wasihi watu. |
| Rais a**na**furahi sana | Rais a**ta**furahi sana. |



## Ziara ya Rais

Ilikuwa siku ya Jumatatu mwezi wa Januari Rais alipotutembelea. Rais wetu alikuja kijijini kukutana na raia. Gari lake lilisimama barabarani.

Rais akasema, “Nawasihi mkae kwa amani na watu wote.” Siku hiyo, wanakijiji walikuwa na furaha sana.

Akimalizia ziara yake, mara tukasikia radi.

Watu wakatorokea madukani.

Kesho yake barabara ilikuwa imejaa maji.

Tamka sauti.

■ j J r R

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: I ju maa - **Ijumaa**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| tu | no | ji | ki | i | do |
| maa | i | ju | n | ma | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Wakati uliopita | Wakati ujao |
|---|---|
| Zakayo **ali**lala kitini | Zakayo **ata**lala kitini. |
| Zakayo **ali**sugua jino | Zakayo **ata**sugua jino. |
| Mama **ali**muona Zakayo | Mama **ata**muona Zakayo. |
| Mama **ali**elekea dukani | Mama **ata**elekea dukani. |

## Jino la Zakayo



Jumamosi asubuhi, Zakayo alilala kitini.
Jino lake lilikuwa linamuuma.
Alilala huku akilisugua jino kwa kidole.
Mara alijikaza kuelekea jikoni.
Huko aliokota jivu na kuliweka kwenye jino.
Mama yake alimuona ameketi jikoni akilia.
Mama alielekea dukani. Akanunua dawa na kumletea.
Akanywa dawa. Jino likatulia.

Tamka sauti.

■ m a u k

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: ma ma - **mama**.

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kaa | ma | mu | ka | m |
| maa | ku | a | kuu | u |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Umoja | Wakati ujao |
|---|---|
| Kaka **aka**amua kuamka | Kaka **waka**amua kuamka. |
| Kaka **aka**muuma kaa | Kaka **waka**wauma kaa. |

## Kaka na Kaa

Kuku akaamua kuamka.

Paka akaamua kuamka.

Mama akaamua kuamka.

Kaka akaamua kuamka.

Kaka akaamua kukaa na kaa.

Kaa akamuuma kaka.

Paka akamuuma kaa.



Tamka sauti.

t T i I n N o O

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: ta mu - **tamu**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ni | m | na | ta | mi |
| mu | ti | i | nu | ma |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Tai a**na**kaa | Tai a**ta**kaa. |
| Kima a**na**kataa | Kima a**ta**kataa. |
| Tai a**na**mtuma | Tai a**ta**mtuma. |
| Konokono a**na**kataa | Konokono a**ta**kataa. |

## Tai na Kima

Tai anakaa na kima mtini.
Tai anataka kununua asali na ini nono.
Tai akamtuma kima.
Kima akakataa.
Tai akaona konokono mtini.
Akamuita na kumtuma.
Konokono akakataa.
Tai akanuna.



Tamka sauti.

w W e E l L h H

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: mi wi li - **miwili**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ki | a | wi | li | wa |
| ka | mi | tu | ha | wi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopita** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Katile a**li**wahukumu | Katile a**ta**wahukumu. |
| Barasa a**li**lia | Barasa a**ta**lia. |
| Wakili a**li**lalamika | Wakili a**ta**lalamika. |
| Hawa a**li**lewa | Hawa a**ta**lewa. |

## Wamiti na Hawa



Wamiti na Hawa walienda sokoni. Walinunua mboga, nyanya na vitunguu.

Wamiti aliona viatu vizuri vya bei ghali.

Alivitamani lakini hakuwa na pesa. Wamiti alivichukua viatu akampa Hawa.

Walishikwa na kupelekwa katika mahakama. Wote walihukumiwa miaka miwili na hakimu. Wamiti na Hawa waliomba msamaha.

Tamka sauti.

■ s S b B y Y z Z

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: sa ba - **saba**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| wa | mo | sti | sa | mi | zi |
| bi | to | ya | ba | ma | s |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| Ni**na**sikia mayowe | Ni**ta**sikia mayowe. |
| Ni**na**tazama moto | Ni**ta**tazama moto. |
| Ni**na**uzima moto | Ni**ta**uzima moto. |
| Ni**na**elekea sebuleni | Ni**ta**elekea sebuleni. |

## Waya wawaka moto

Tulisikia mayowe tukiwa sebuleni.



"Tokeni!" Baba akasema.

Sote tukatoka.

Kutazama tukaona moto ukiwaka sana.

Waya wa stima jikoni mwa jirani wetu uliwaka moto.

Sote tukawa na wasiwasi sana.

Wazimamoto wakafika.

Wakauzima moto uliokuwa umeenea.

Mioyo yetu ikatulia, tukaelekea sebuleni tena.

Tamka sauti.

g G d D j J r R

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno. Kwa mfano: Ju ni - **Juni**


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ni | ma | ju | se | mba |
| go | a | sti | de | mbe |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| **wana**soma | **wali**soma |
| **wana**furahia | **wali**furahia |
| **wana**rudi | **wali**rudi |
| **wana**saidia | **wali**saidia |

## Hali ya Hewa

Januari na Februari kuna joto na jua kali. Watoto wanasoma kwa bidii sana. Aprili ni likizo. Baada ya likizo watoto husoma miezi ya Mei, Juni hadi Julai. Agosti huwa likizo tena. Watoto hufurahia kusaidia wazazi. Wao hurudi kusoma kwa miezi mitatu hadi likizo ya sikukuu ya Disemba.



Tamka sauti.

**p** **g** **d**

Soma sauti za herufi na silabi.

p e p i p u p o

**pe** **pi** **pu** **po**

Soma silabi na maneno.

pa sa ka Pa te Pe te ro pa pa

**pasaka** **Pate** **Petero** **papa**

Tamka sauti.

**P** **p**

Soma silabi.

**e** **a**

**we** **wa**

**pwe** **pwa**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li ona wa ki tumia

**waliona** **wakitumia**

wa li tumia i li po wadia

**walitumia** **ilipowadia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| **Huyu** ni punda **mmoja** | **Hawa** ni punda **wawili.** |
| **Huyu** ni papa **mmoja** | **Hawa** ni papa **watatu.** |
| **Huyu** ni pweza **mmoja** | **Hawa** ni pweza **wanne.** |
| **Huyu** ni samaki **mmoja** | **Hawa** ni samaki **watano.** |



## Sikukuu ya Pasaka

Sikukuu ya pasaka ilipowadia, Petero na wazazi wake walitoka Pate na kuelekea Faza. Walitumia magari mawili hadi Mpeketoni. Wakatumia dau kuvukia Bahari Hindi hadi kisiwani Faza. Kule kisiwani, waliona watu sita wakitumia punda kubebea mizigo na watu. Pia waliona papa na pweza. Papa walikuwa ishirini na pweza walikuwa kumi na wanne.

Tamka sauti.

■ **f F** **p P**

Soma sauti za herufi na silabi.

● f i f e f o f a

**fi** **fe** **fo** **fa**

Soma silabi na maneno.

▬ a li fa u lu fa ra si pi ki pi ki fo le ni

**alifaulu** **farasi** **pikipiki** **foleni**

Tamka sauti.

▲ **F** **f**

Soma sauti za herufi na silabi.

⬬ p e f e k e w e

**pe** **fe** **ke** **we**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ki li furahi

**kilifurahi**

wa li furahi

**walifurahi**

wa m salimie

**wamsalimie**


wa li safiri

**walisafiri**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hii ni pikipiki **moja** | Hizi ni pikipiki **mbili**. |
| Hii ni matatu **moja** | Hizi ni matatu **tatu**. |
| Hii ni baiskeli **moja** | Hizi ni baiskeli **nne**. |
| Hii ni meli **moja** | Hizi ni meli **tano**. |



## Matokeo ya Apese

Apese alifaulu mtihani wa darasa la nane. Alipata alama mia nne hamsini.

Kijiji kizima kilifurahi sana.

Wanakijiji walifurahi na kupiga vigelegele.

Walisafiri kwa kutumia farasi wanne, mabasi mawili na pikipiki kumi na mbili. Wengine walisafiri kwa kutumia matatu tano na baiskeli ishirini na tano.

Wakapiga foleni ili wamsalimie Apese.

Wazazi wake walifurahi kwa matokeo ya mtoto wao.

Tamka sauti.

■ p P f F

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: pa sa ka - **pasaka**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ni | pa | fa | si | ra | fi |
| ba | ha | na | ka | sa | ri |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| enda | rudi |
| mchana | usiku |
| baba | mama |
| dada | kaka |



## Usafiri

Kila mtu hutamani kusafiri kwa njia za kifahari. Njia hizi ni kama eropleni, magari na meli. Nikiwa na safari fupi, mimi husafiri kwa miguu mara mbili kwa wiki. Kusafiri kwa miguu kuna faida kwenye mwili wa binadamu. Zaidi ya hayo, msafiri hatumii hela zozote kusafiri. Je, wewe husafiri kwa miguu mara ngapi kwa wiki?

Tamka sauti.

■ **v** **p** **f**

Soma sauti ya herufi na silabi.

● v e v i v u v a

**ve** **vi** **vu** **va**

Soma silabi na maneno.

▬ vi ji to wa vu vi vi bo ko ma de vu

**vijito** **wavuvi** **viboko** **madevu**

Tamka sauti.

▲ **V** **v**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ f o v o f e v e

**fo** **vo** **fe** **ve**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ya li malizika a ka wa ita

**yalimalizika** **akawaita**

vi ka haribiwa wa li po kata

**vikaharibiwa** **walipokata**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hiki ni **ki**jito | Hivi ni **vi**jito. |
| Hiki ni **ki**lima | Hivi ni **vi**lima. |
| Hiki ni **ki**boko | Hivi ni **vi**boko. |
| Hiki ni **ki**ota | Hivi ni **vi**ota. |



## Athari za ukataji wa miti

Kijijini Taita kulikuwa na vijito na vilima.
Vijana wa huko walikuwa wavuvi wa samaki.
Watu walipokata miti, maji yalimalizika vijitoni.
Viboko na samaki wakafa.
Viota vikaharibiwa.
Mzee Madevu akawaita watu na kusema, "Tunahitaji kupanda miti, ili tupate maji visimani."

Tamka sauti.

**sh** **v** **f**

Soma sauti ya herufi na silabi.

sh o — **sho**
sh e — **she**
sh i — **shi**
sh a — **sha**

Soma silabi na maneno.

shu le ni — **shuleni**
ni sha ni — **nishani**
di ri sha ni — **dirishani**
m ko ro sho — **mkorosho**

Tamka sauti.

**Sh** **sh**

Soma sauti ya herufi na silabi.

sh i — **shi**
s i — **si**
sh u — **shu**
s u — **su**

Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka simama — **akasimama**
wa ka shikana — **wakashikana**
wa li washa — **waliwasha**
wa ka amua — **wakaamua**

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Neno** | **Matumizi ya -ni** |
|---|---|
| shule | shule**ni** |
| dirisha | dirisha**ni** |
| arasa | darasa**ni** |
| kijiji | kijiji**ni** |



## Aisha na Shiko wazawadiwa

Aisha alifika shuleni mapema. Akasimama dirishani na kutazama Shumila akikariri shairi. Mara Shiko akatokea. Wakashikana mikono kwa furaha. Shiko akasema, "Hujambo Aisha?" Aisha akajibu, "Sijambo. U hali gani Shiko?" "Njema," Shiko akajibu. Shumila akasikia kelele akashtuka. Mara akawaona Shiko na Aisha. Shiko akasema, "Pole." Aisha akasema, "Samahani."

Kisha wakaamua kufagia karibu na mkorosho. Baadaye waliwasha majani na takataka moto.

Siku hiyo, mwalimu mkuu aliwapa nishani na shada la maua.

Tamka sauti.

■ v V f F sh

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: vi bo ko - **viboko**

★

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| fo | di | shi | bo | ri | sha | ma |
| ko | ni | ji | to | le | li | vi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Dereva **ali**simama | **Ma**dereva **wali**simama. |
| Dereva **ali**furahi | **Ma**dereva **wali**furahi. |
| Dereva **ali**ogopa | **Ma**dereva **wali**ogopa. |
| Dereva **ali**lala | **Ma**dereva **wali**lala. |



## Dereva na kima

Siku moja dereva mvivu alisimamisha gari lake karibu na barabara. Akala viazi vitamu na uji. Mara akajifunika kwa vazi lake kisha akalala fofofo. Kima watano wakamvamia. Walisukuma gari lake hadi msituni. Dereva alipoamka alijikuta katikati ya miti msituni. Kima walipoona dereva ameamka wakaogopa na kutorokea msituni.

Tamka sauti.

■ **ny** **v** **sh**

Soma sauti ya herufi na silabi.

● ny a ny i ny e ny u

**nya** **nyi** **nye** **nyu**

Sarufi: Soma silabi na maneno.

▬ nyu ki Nya nyi ro

**nyuki** **Nyanyiro**

wa nya ma nyo ro ro

**wanyama** **nyororo**

Tamka sauti.

▲ **Ny** **ny**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ ny a n a n e ny e

**nya** **na** **ne** **nye**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ wa ka kaza wa ka m tafuta

**wakakaza** **wakamtafuta**


a li kariri wa ka toroka

**alikariri** **wakatoroka**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mtu **a**liishi hapa | Watu **wa**liishi hapa. |
| Mtu **a**limtafuta sana | Watu **wa**liwatafuta sana. |
| Mtu **a**likaza mguu wake | Watu **wa**likaza miguu yao. |
| Mtu **a**likariri shairi | Watu **wa**likariri mashairi. |



## Nyamari na nyuki

Nyamari aliishi kijijini Nyanyiro.
Yeye alijua kukariri mashairi.
Alijua mashairi ya wanyama na nyuki.
Watu wabaya wenye nyororo wakaja na kumteka nyara Nyamari.
Wanakijiji wa Nyanyiro walimtafuta hata msituni.Watu wabaya wakakaza mikono na miguu kwa nyororo. Nyamari alikariri shairi la nyuki.
Nyuki wakaja na kuwauma wale watu wabaya.
Wakatoroka huku wakilia.

Tamka sauti.

■ **dh** **ny** **v**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● dh a dh e dh i dh o

**dha** **dhe** **dhi** **dho**

Soma silabi na maneno.

▬ Go dha na bi dha a fe dha dha ha bu

**Godhana** **bidhaa** **fedha** **dhahabu**

Tamka sauti.

▲ **Dh** **dh**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ dh u d u dh i d i

**dhu** **du** **dh i** **di**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ki na meta meta a ka m pasua

**kinametameta** **akampasua**


a li po fika a ka nunua

**alipofika** **akanunua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Samaki huyu ni **m**dogo | Samaki hawa ni **wa**dogo. |
| Samaki huyu ni **m**tamu | Samaki hawa ni **wa**tamu. |
| Samaki huyu ni **m**refu | Samaki hawa ni **wa**refu. |
| Samaki huyu ni **m**zuri | Samaki hawa ni **wa**zuri. |



## Godhana atajirika

Godhana alitaka kununua bidhaa tofauti tofauti.
Siku hiyo hakuwa na fedha za kutosha.
Jioni moja, akanunua samaki mdogo na dania.
Alipofika kwake, alimweka samaki mezani, kisha akampasua.
Godhana akapata kijiwe kidogo ndani ya samaki.
Akakiosha kijiwe mara akaona kinametameta.
Alipojua ni dhahabu alifurahi sana.
Godhana akaiuza dhahabu hiyo, akatajirika.

Tamka sauti.

■ ny Ny dh Dh

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: nyo ro ro - **nyororo**

★

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| nyu | nya | ki | ra | nyo | dha | ha |
| ma | si | wa | ro | re | u | bu |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **a**liugua | **wa**liugua |
| **a**liwapa | **wa**liwapa |
| **a**likuwa | **wa**likuwa |
| **a**liparara | **wa**liparara |

## Usafi



Watoto wa Shinyanya hawakuwa safi. Hawakuoga wala kusugua meno. Nyayo zao zilipasuka hata zikawa na vidonda. Miili yao pia ilipararara. Kwao hakukuwa safi. Nyuki, nyigu, panya na nyoka walihamia huko. Watoto hawa walikuwa na minyoo na waliugua. Nyanya yao aliwapa dawa na kuwashauri wawe safi.

Tamka sauti.

■ **th** **ny** **dh**

Soma sauti ya herufi na silabi.

● th a th u th i th e

**tha** **thu** **thi** **the**

Soma silabi na maneno.

▬ the la thi ni the ma ni ni

**thelathini** **themanini**

tha ma ni dha ti

**thamani** **dhati**

Tamka sauti.

▲ **Th** **th**

Soma sauti ya herufi na silabi.

⬬ th a t a t o th o

**tha** **ta** **to** **tho**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a li po jua a me mu ibia

**alipojua** **amemuibia**


ha ja thubutu u ka isha

**hajathubutu** **ukaisha**

Sarufi: Soma maneno haya.

◆

| **Neno** | **Kinyume** |
|---|---|
| lala | amka |
| fupi | refu |
| rafiki | adui |
| keti | simama |



## Nyati na Nyoka

Nyati na Nyoka walikuwa marafiki wa dhati.
Walikaa pamoja kila wakati.
Nyoka alikuwa na miaka themanini.
Nyati alikuwa na miaka thelathini.
Nyoka alikuwa na vitu vya thamani.
Siku moja nyati akamuibia nyoka.
Nyoka alipojua kuwa nyati amemuibia alikasirika sana.
Hapo hapo urafiki wao ukaisha.
Tangu siku hiyo nyati hajathubutu kukaa karibu na nyoka tena.

Tamka sauti.

**ch** **th** **dh**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

ch a ch i ch o ch e

**cha** **chi** **cho** **che**

Soma silabi na maneno.

chu i chu ra cha tu m che zo

**chui** **chura** **chatu** **mchezo**

Tamka sauti.

**Ch** **ch**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

ch u j u h u ch o

**chu** **ju** **hu** **cho**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li cheza a ka hesabu


**walicheza** **akahesabu**

a ka mweka a li kasirika

**akamweka** **alikasirika**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Chatu **huyu** ni mmoja 1 | Chatu **hawa** ni kumi. 10 |
| Chiriku **huyu** ni mmoja 1 | Chiriku **hawa** ni ishirini. 20 |
| Chui **huyu** ni mmoja 1 | Chui **hawa** ni hamsini. 50 |
| Chura **huyu** ni mmoja 1 | Chura **hawa** ni sitini. 60 |



## Mchezo wa wanyama

Chatu, Chura na Chui waliishi kwenye kichochoro.
Siku moja walicheza mchezo wa kuhesabu nyota.
Chatu alihesabu na kupata nyota kumi tu.
Chui naye alihesabu kutoka kumi hadi ishirini.
Chura akahesabu kutoka thelathini, arobaini, hamsini, sitini, sabini, themanini, tisini hadi mia moja.
Chui alikasirika sana.
Akamweka Chura kwenye chupa.

Soma sauti.

■ th Th ch Ch

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: the lu ji – **theluji**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| the | ni | ji | cha | ra | che |
| ma | lu | tha | i | che | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Wakati uliopita | Wakati ujao |
|---|---|
| Chui a**li**kasirika | Chui a**ta**kasirika. |
| Chui a**li**mweka | Chui a**ta**mweka. |
| Chatu a**li**hesabu | Chatu a**ta**hesabu. |
| Chura a**li**cheza | Chura a**ta**cheza. |

## Nyororo za dhahabu



Tabitha alikuwa na nyororo kumi za dhahabu. Chebet akasema, "Ukinipatia nyororo hizi za dhahabu nitazifanya ziwe thelathini." Tabitha akasema, "Hata kama utazifanya ziwe themanini sikupi." Chebet hakuacha kuuliza kuhusu nyororo hizo. Tabitha alijua thamani ya nyororo zake. Kutoka siku hiyo hakuthubutu kuziweka hadharani tena.

Tamka sauti.

**gh** **th** **ch**

Soma sauti ya herufi na silabi.

gh e | gh o | gh u | gh a

**ghe** **gho** **ghu** **gha**

Soma silabi na maneno.

gho ro fa | gha li | gha si a | gha ra ma

**ghorofa** **ghali** **ghasia** **gharama**

Tamka sauti.

**Gh** **gh**

Soma sauti ya herufi na silabi.

gh i | h i | g i | k i

**ghi** **hi** **gi** **ki**

Soma sehemu za neno na neno lote.

tu li shangaa | wa ka mu umiza

**tulishangaa** **wakamuumiza**

ya ka raruka | vi li onekana

**yakararuka** **vilionekana**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja -ake** | **Wingi -ao** |
|---|---|
| Hili ni vazi **lake** | Haya ni **ma**vazi **yao.** |
| Hili ni shati **lake** | Haya ni **ma**shati **yao.** |
| Hili ni koti **lake** | Haya ni **ma**koti **yao.** |
| Hili ni gauni **lake** | Haya ni **ma**gauni **yao.** |



## Adhabu ya mwizi

Kulitokea ghasia kijijini kwetu.
Mimi na wazazi wangu tuliishi katika ghorofa ya tatu.
Tulishangaa kuona mtu akifukuzwa. Polisi walimkamata.
Mavazi yake yakararuka.
Suruali yake ikapasuka vipande vikaanguka.
Kofia na viatu vyake vilionekana kuwa ghali sana.
Baadaye jirani akasema kuwa mwizi huyo alikuwa ameiba vitu sokoni.

Tamka sauti.

ng gh th

Soma sauti ya herufi na silabi.

ng e ng u ng o ng a

**nge** **ngu** **ngo** **nga**

Soma silabi na maneno.

we ngi ne shi ngo ni ma ko nge sha nga

**wengine** **shingoni** **makonge** **shanga**

Tamka sauti.

**Ng** **ng**

Tamka sauti ya herufi na silabi

ng a ng' a g a k a

**nga** **ng'a** **ga** **ka**

Soma sehemu za neno na neno lote.

vi li kuwa ha wa ku vaa

**vilikuwa** **hawakuvaa**

ya me badilika wa li beba

**yamebadilika** **walibeba**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja -angu | Wingi -etu |
|---|---|
| Huyu ni baba **yangu** | Hawa ni baba **zetu.** |
| Huyu ni babu **yangu** | Hawa ni mababu **zetu.** |
| Huyu ni bibi **yangu** | Hawa ni mabibi **zetu.** |
| Huyu ni mama **yangu** | Hawa ni mama **zetu.** |



## Mavazi ya zamani

Zamani mababu na mabibi zetu hawakuvaa mavazi ya bei ghali.
Walivaa nguo za ngozi kiunoni.
Pia walivaa shanga za rangi mbalimbali shingoni.
Viatu vyao vilikuwa vya miti, ngozi na mkonge.
Wengine walibeba rungu ili kuonyesha cheo au heshima.
Siku hizi mambo yamebadilika.
Watu wanavaa watakavyo.
Mavazi hayana heshima wala kujali utamaduni wetu.

Soma sauti.

ng Ng gh Gh

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: ngo zi - **ngozi**.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| gha | sha | li | o | ngo | ra |
| nga | ru | ngu | zi | ngi | ndi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. Nili**kula** chumbani.
2. Nili**cheza** uani.
3. Nili**keti** ghalani.
4. Nili**kimbia** shuleni.

## Mavazi ya mama Fatuma



Fatuma alikuwa chumbani. Mvua ikaanza kunyesha kwa ghafla. Kukawa na gharika. Mama alikuwa ghalani akitoa nafaka. Mavazi yake yalikuwa uani. Nikakimbia na kutoa rinda, gauni, sketi, kamisi na blauzi ya mama. Kwa kawaida mavazi ya mama huwa ghali sana.

Tamka sauti.

■ **ng’** **gh** **ng**

Soma sauti ya herufi na silabi.

● ng’ a ng’ i ng’ u ng’ o

**ng’a** **ng’i** **ng’u** **ng’o**

Soma silabi na maneno.

▬ ng’o mbe ng’a mbo Ng’a ng’a se ng'e nge

**ng’ombe** **ng’ambo** **Ng’ang’a** **seng'enge**

Tamka sauti.

▲ **Ng’** **ng’**

Soma sauti ya herufi na silabi.

⬬ ng’ a ng a ng’ e ng e

**ng’a** **nga** **ng’e** **nge**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku hudhuria a ka ng’oa

**kuhudhuria** **akang’oa**


ku ng’a ra a li nunua

**kung’ara** **alinunua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ndama huyu ni **mwe**usi | Ndama hawa ni **we**usi. |
| Nyati huyu ni **mwe**usi | Nyati hawa ni **we**usi. |
| Duma huyu ni **mwe**upe | Duma hawa ni **we**upe. |
| Ngamia huyu ni **mwe**upe | Ngamia hawa ni **we**upe. |



## Ng’ang’a auza ng’ombe

Ng’ang’a aliishi peke yake ng’ambo ya mto.
Siku moja, alitaka kuhudhuria maonyesho ya kilimo sokoni.
Siku hiyo alivaa nguo nyeupe za kung’ara.
Alipofika mtoni, aling’oa mti ili apime kina cha maji.
Alipovuka mto, Ng’ang’a aliuza ng’ombe wake.
Baadaye alinunua seng’enge na bidhaa mbalimbali.
Alirudi kwake akiwa na furaha nyingi.

Tamka sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i a | o a | e a | u a |
| **ia** | **oa** | **ea** | **ua** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a li zo e a | ha ku tii | a ka m zu i a |
| **alizoea** | **hakutii** | **akamzuia** |
| ku zo a | u o ngo | zo e a |
| **kuzoa** | **uongo** | **zoea** |

Soma sauti ya herufi na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a o | u i | a e | a u |
| **ao** | **ui** | **ae** | **au** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha ku tii | a ka futwa |
| **hakutii** | **akafutwa** |
| a ka m zuia | a ka puuza |
| **akamzuia** | **akapuuza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja -ake** | **Wingi -ao** |
|---|---|
| Yule ni **mwa**limu wake | Wale ni **wa**limu wao. |
| Yule ni **m**tumishi wake | Wale ni **wa**tumishi wao. |
| Yule ni **m**shirika wake | Wale ni **wa**shirika wao. |



## Juma Mvivu

Juma alikuwa mfanyikazi shambani mwa shule. Msimamizi wake akasema, “Acha uvivu.” Juma hakutii. Msimamizi akamzuia kuzoa takataka shambani. Juma akasema uongo ili apewe kazi yake tena. Msimamizi wake akasema asubiri uamuzi wa kamati ya shule. Juma bado alipuuza maagizo. Mwalimu mkuu alimfuta kazi.

Tamka sauti.

■ **ng** **Ng'**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: si ki a - **sikia**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ng'o | ng'a | ki | a | ri | ma |
| mbo | mbe | si | sa | fa | nge |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| **Wakati uliopo** | **Wakati uliopita** |
|---|---|
| Juma **ana**zoea | Juma **ali**zoea |
| King'ori **ana**enda | King'ori **ali**enda |
| Marangi **ana**elekea | Marangi **ali**elekea |

## Marangi aenda kwa King'ori

Marangi alifunga safari kwenda kwa King'ori. Yeye na King'ori wakala mayai ya kukaanga. Walipomaliza, walielekea eneo la wazi kulikokuwa na maua. Walitoa mkeka na kuulalia. Waliwaona kuku waliokuwa wameangua vifaranga.



Mwewe alipowakaribia, walimtimua.

Soma sauti ya herufi na silabi.

■ a o    i o    e e    u o

**ao**    **io**    **ee**    **uo**

Soma silabi na maneno.

● u ba o    mwe u si    ki cho nge o

**ubao**    **mweusi**    **kichongeo**

Ne re a    ki fu ti o    shi ka moo

**Nerea**    **kifutio**    **shikamoo**

Soma sauti ya herufi na silabi.

▲ e o    o u    o i    o e

**eo**    **ou**    **oi**    **oe**

Soma sehemu za neno na neno lote.

⬬ a ki ingia    a na itwa

**akiingia**    **anaitwa**


hu mu amkua    hu tumia

**humuamkua**    **hutumia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

★

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hiki ni **ki**tabu **ch**eusi. | Hivi ni **vi**tabu **vy**eusi. |
| Hiki ni **ki**futio **ch**eusi. | Hivi ni **vi**futio **vy**eusi. |
| Hiki ni **ki**chongeo **ch**eupe. | Hivi ni **vi**chongeo **vy**eupe. |
| Hiki ni **ki**tabu **ch**eupe. | Hivi ni **vi**tabu **vy**eupe. |



## Darasa la Maria

Maria yuko katika darasa la kwanza.
Mwalimu wake anaitwa Nerea.
Nerea akiingia darasani, wanafunzi humuamkua, "Shikamoo?" Mwalimu hujibu, "Marahaba wanafunzi."
Darasa lao ni kubwa.
Kwenye kuta kuna saa ya duara na chati. Kwenye chati kuna michoro yenye maumbo mbalimbali. Kwa mfano, pembe tatu, mraba na duara.
Darasa lina ubao mweusi wa umbo la mstatili.
Mwalimu wao hutumia chaki kuandikia ubaoni.
Kila mwanafunzi huwa na kitabu, kalamu, kifutio na pia kichongeo.

Tamka sauti ya herufi na silabi.

■ b a d a p a b o

**ba** **da** **pa** **bo**

Soma silabi na maneno.

● Ki o ko ta bi a

**Kioko** **tabia**

wa na tu li a ki ra nja

**wanatulia** **kiranja**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

▲ b e b u p e p u

**be** **bu** **pe** **pu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

⬬ a li kusanya a li hakikisha

**alikusanya** **alihakikisha**

a li furahishwa wa li po chagua

**alifurahishwa** **walipochagua**

Sarufi: Soma maneno haya.

★

| Wakati uliopo | Wakati uliopita |
|---|---|
| **ana**mpenda | **ali**mpenda |
| **ana**furahisha | **ali**furahisha |
| **ana**hakikisha | **ali**hakikisha |
| **ana**chagua | **ali**chagua |



## Kiranja wetu

Kioko alikuwa kiranja wa darasa la kwanza.
Alihakikisha wanafunzi wanatulia darasani.
Alikusanya na kumsaidia mwalimu kubeba vitabu vya wanafunzi.
Kabla ya mwalimu kuingia darasani, Kioko alihakikisha wanafunzi wametulia.
Mwalimu alifurahishwa na kazi ya Kioko.
Wanafunzi pia walimpenda kwani alikuwa na tabia nzuri.
Kila walipochagua kiranja, Kioko alichaguliwa.

Soma sauti za herufi na silabi.

i a o o i o e a u a

**ia** **oo** **io** **ea** **ua**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: u ba o - **ubao**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| o | ba | bu | li | mu |
| pi | u | ki | ta | bi |
| da | ti | wa | fu | cha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. Judi *ali***soma** kitabu.
2. Rono *ali***chonga** penseli.
3. Njoki *ali***futa** ubao.
4. Bari *ali***chora** chati.

## Somo la wanyama



Ijumaa iliyopita, wanafunzi wa darasa la kwanza walisoma kuhusu wanyama. Mwalimu alitumia chati ya wanyama kufunzia somo hilo. Kwenye chati kulichorwa ngamia, kondoo, ng'ombe, mbuzi na jimbi au jogoo. Wanafunzi waliimba wimbo kuhusu wanyama tofauti. Baadaye mwalimu aliwaletea redio. Wakasikiza somo la redio. Wanafunzi walifurahi sana.

Tamka sauti.

m t s p

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| ta | sa | pa | me |
| mta | msa | mpa | mme |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | mi go mba | cha mbo |
| **mkulima** | **migomba** | **chambo** |
| m vu vi | Ka je mbe | mi e mbe |
| **mvuvi** | **Kajembe** | **miembe** |

Tamka sauti.

m f b k v

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | u | u |
| fa | ba | ku | vu |
| mfa | mba | mku | mvu |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li penda | a li tumia |
| **alipenda** | **alitumia** |
| a li kuwa | a li ji funga |
| **alikuwa** | **alijifunga** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Huyu ni **m**zee | Hawa ni **wa**zee. |
| Huyu ni **m**kulima | Hawa ni **wa**kulima. |
| Huyu ni **m**vuvi | Hawa ni **wa**vuvi. |
| Huyu ni **mwa**limu | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **mwa**nafunzi | Hawa ni **wa**nafunzi. |



## Kajembe

Mzee Kajembe aliishi katika kijiji cha Mbalambala.
Kajembe alikuwa mkulima na mvuvi hodari sana. Kila siku alijifunga kilemba na kuelekea mtoni.
Akiwa mtoni, Kajembe alipenda kuimba na kucheza na firimbi yake.
Mto huo ulikuwa na samaki na mamba wengi sana.
Mara nyingi alitumia chambo na fimbo kuvua samaki.
Pia alikuwa na shamba la migomba na miembe.
Mzee Kajembe husafirisha samaki hadi sokoni. Kule sokoni yeye huuza samaki kwa wateja wengi.

Tamka sauti.

| n | d | j | z |
|---|---|---|---|

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | e |
| **da** | **ja** | **za** | **de** |
| **nda** | **nja** | **nza** | **nde** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki ba nda<br>**kibanda** | hu pe nda<br>**hupenda** | bo nde<br>**bonde** |
| ki wa nda<br>**kiwanda** | ma a nda zi<br>**maandazi** | ki na nda<br>**kinanda** |

Tamka sauti.

| t | m | ch | b |
|---|---|---|---|

Soma silabi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **i** | **i** |
| **ta** | **ba** | **ti** | **chi** |
| **nta** | **mba** | **mti** | **nchi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i li yo kuwa<br>**iliyokuwa** | ku li kuwa<br>**kulikuwa** |
| zi li zo shika<br>**zilizoshika** | ni li enda<br>**nilienda** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hili ni bonde | Haya ni **ma**bonde. |
| Hili ni andazi | Haya ni **ma**andazi. |
| Hili ni gari | Haya ni **ma**gari. |
| Hili ni banda | Haya ni **ma**banda. |



## Kaka Banda

Ndugu yangu Banda anaishi kwenye kibanda karibu na bonde la nzi, karibu na soko la Suswa.
Banda hufanya kazi katika kiwanda cha mwananchi.
Kila asubuhi yeye hupenda kula maandazi kwa supu ya kunde. Yeye hupata vyakula hivi sokoni.
Juzi nilienda nyumbani kwake.
Huko niliona kitanda, kinanda na kalenda iliyokuwa na picha ya bundi. Vifaa hivi vilitengenezwa na rafiki yake Janda. Janda ni fundi maarufu huko Bondeni. Kule Bondeni kulikuwa na matope yaliyoshikana kama gundi.

Tamka sauti.

ng Ng gh Gh

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: ngo zi - **ngozi**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| gha | sha | li | o | ngo | ra |
| nga | fo | ngu | fa | zi | ngi |
| ndi | ghe | gho | ru | ni | mbu |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | Matumizi ya "ni" |
|---|---|
| uwanja | uwanja**ni** |
| nyumba | nyumba**ni** |
| shamba | shamba**ni** |
| kiwanda | kiwanda**ni** |

## Umuhimu wa Mbuzi



Mbuzi ni mnyama mwenye manufaa mengi kwa wafugaji. Mbolea ya mbuzi ni nzuri kwa ukulima. Ngozi ya mbuzi hutumiwa kutengenezea viatu na mikoba. Mbuzi wa kike hutoa maziwa yanayofaidi mwili wa binadamu. Nyama yake ni tamu sana. Watu wengine huchoma na kupika nyama ya mbuzi. Wengine huwauza sokoni ili kupata pesa. Ni muhimu sana kutunza mbuzi na wanyama wote wa kufugwa.

Tamka sauti.

■ **y** **v** **p**

Soma sauti ya herufi na silabi.

● 

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **o** | **a** | **u** |
| **ya** | **yo** | **ya** | **yu** |
| **vya** | **vyo** | **pya** | **vyu** |

Soma silabi na maneno.

▬

| | | |
|---|---|---|
| vi pya | o vyo o vyo | vyu ma |
| **vipya** | **ovyoovyo** | **vyuma** |
| vyu ngu | m guu | pi ngu |
| **vyungu** | **mguu** | **pingu** |

Tamka sauti.

▲ **m** **f** **p**

Soma sauti ya herufi na silabi.

⬬

| | | |
|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** |
| **ya** | **ya** | **ya** |
| **mya** | **fya** | **pya** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★

| | |
|---|---|
| wa li m funga | i ka mu umiza |
| **walimfunga** | **ikamuumiza** |
| ha ku tarajia | wa ka fyatua |
| **hakutarajia** | **wakafyatua** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Huyu ni **m**tu **m**zuri | Hawa ni **wa**tu **wa**zuri. |
| Huyu ni mbuzi **m**zuri | Hawa ni mbuzi **wa**zuri. |
| Huyu ni **m**nyama **m**baya | Hawa ni **wa**nyama **wa**baya. |
| Huyu ni kondoo **m**baya | Hawa ni kondoo **wa**baya. |



## Jambazi akamatwa

Oga alikuwa jambazi hatari.
Aliiba vitu vipya na kuviuza ovyoovyo.
Siku moja, Oga aliingia dukani kimyakimya na kuiba vyuma na vyungu vya dhahabu.
Alipoingia tu, king'ora kikaanza kulia.
Oga hakutarajia hayo.
Akaanza kutoroka. Polisi wakafyatua risasi ikamuumiza mguu.
Wakamkamata na kumpeleka hospitalini.
Baadaye walimfunga pingu na kumfungia seli.

Soma sauti.

w k t b

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| **kwa** | **twa** | **mwa** | **bwa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | m ku bwa | mi chu ngwa |
| **mbwa** | **mkubwa** | **michungwa** |
| bwa wa | ku nywa | ja ngwa ni |
| **bwawa** | **kunywa** | **jangwani** |

Soma sauti.

w sh z ny ng

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | a | a | a |
| wa | wa | wa | wa |
| **shwa** | **zwa** | **nywa** | **ngwa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a ki bweka | i li po pulizwa |
| **akibweka** | **ilipopulizwa** |
| a ka tuzwa | a ka twa a |
| **akatuzwa** | **akatwaa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mbwa huyu ni **m**kubwa | Mbwa hawa ni **wa**kubwa. |
| Mamba huyu ni **m**kubwa | Mamba hawa ni **wa**kubwa. |
| Mbwa huyu ni **m**kali | Mbwa hawa ni **wa**kali. |
| Mnyama huyu ni **m**dogo | Wanyama hawa ni **wa**dogo. |



## Mashindano ya mbio

Punde tu firimbi ilipopulizwa, Sanaipei alipewa mwenge ndipo tukaanza mbio. Mbio zilianza uwanjani, kupitia mtoni kuelekea jangwani.

Njiani tuliona michungwa, miembe na mipera.

Pia tuliona mbwa mkubwa akibweka karibu na bwawa la maji.

Tulitamani kunywa maji, kwa sababu tulihisi kiu.

Mwalimu akatuambia bwawa lilikuwa na mamba wengi.

Tukatoroka kuelekea jangwani.

Sanaipei akawa wa kwanza.

Akatuzwa medali ya dhahabu.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: che nza - **chenza**

★

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **ku** | **mbwa** | **ma** | **ngu** | **che** | **wa** | **nza** | **ngwa** |
| **nywa** | **vyu** | **na** | **bwa** | **chu** | **zwa** | **ja** | **shwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Hiki ni **ch**umba kidogo | Hivi ni **vy**umba vidogo. |
| Hiki ni **ch**eti kikubwa | Hivi ni **vy**eti vikubwa. |
| Hiki ni **ch**oo kirefu | Hivi ni **vy**oo virefu. |
| Hiki ni **ch**akula kingi | Hivi ni **vy**akula vingi. |

## Mvua ya mawe



Siku moja, kulinyesha mvua ya mawe. Watoto wakafurahia kumumunya na kuchezea barafu kimyakimya. Barafu iliwaletea kikohozi. Mama akawasikia watoto wakikohoa. Akawaita nyumbani. Akawapa adhabu ya kufyeka nyasi. Walifyeka nyasi hadi vipaji vyao vikajaa jasho. Baadaye waliomba msamaha. Pia waliahidi kuwa hawangerudia kosa hilo tena.

Soma sauti.

p f v sh

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.


Kwa mfano: shu le - **shule**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| shu | vu | pa | m | fu |
| ka | jaa | a | pi | le |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| darasa **moja** | 1 | madarasa **sita** | 6 |
| | | madarasa **matano** | 5 |
| kanisa **moja** | 1 | makanisa **mawili** | 2 |
| | | makanisa **saba** | 7 |

## Paa la shule yetu



Kuna shule moja tu kijijini mwetu. Wiki jana, upepo mkali uliharibu paa la darasa letu. Hivi sasa, sote tunasomea kanisani.

Lakini shida hii ni ya muda mfupi tu.

Mheshimiwa mbunge wetu, ametuma bahasha ya pesa.

Wazazi nao watakuja kesho shuleni kuchanga pesa zaidi.

Watanunua vifaa na kurekebisha paa hilo.

Soma sauti.

▲ ny dh ch th

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: che ma - **chema**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| che | ta | si | nyo | na |
| ma | cha | ku | m | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● 1. Kitabu kiko **juu ya** meza. 2. Kiatu kiko **chini ya** kiti.





## Chebet



Chebet ni msichana nadhifu. Yeye havai nguo za bei ghali. Anatamani saa ya dhahabu inayometameta kama nyota. Kila siku Chebet huoga na kuchana nywele mara moja, mbili, hata tatu. Yeye habaki nyuma kwa usafi, masomo na michezo. Vilevile, yeye hula lishe bora. Anajua uchafu unaweza kumdhuru. Kila mara akitoka chooni, Chebet hunawa mikono mara nyingi.

Soma sauti.

■ **gh** **ng** **ng'**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: si ku - **siku**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| gha | me | tu | ku | a |
| si | wa | li | gha | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Umoja - hii | Wingi - hizi |
|---|---|
| Nyumba **hii** ya ghorofa | Nyumba **hizi** za ghorofa. |
| Bendera **hii** imezeeka | Bendera **hizi** zimezeeka. |
| Pazia **hii** ni ghali | Pazia **hizi** ni ghali. |
| Sakafu **hii** ni chafu | Sakafu **hizi** ni chafu. |

## Nyumba ya ghorofa



Mwakio alisema, “Nyumba hii ya ghorofa imezeeka. Lakini pazia hii ni ghali na maua haya yanang’ara. Bendera inayopepea kwenye paa ilitoka ng’ambo.” Aliendelea, “Leo ni siku ya kung’ang’ania ugavana. Nitautoa ufunguo huu kwa yule atakayeshinda.” Kendi alishinda. Akapewa ufunguo. Akafungua nyumba na kutulia mezani, huku watu wakishangilia.

Tamka sauti.

▲ **m** **b** **n** **d**

Soma sauti ya herufi na silabi.

m b a n d a n d e n d i

**mba** **nda** **nde** **ndi**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: nda ni - **ndani**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ndi | tu | zi | nda | li |
| le | mba | ni | ye | mu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja -angu | Wingi -etu |
|---|---|
| **Hiki** ni **ki**tanda changu. | **Hivi** ni **vi**tanda vyetu. |
| **Hiki** ni **ki**banda changu. | **Hivi** ni **vi**banda vyetu. |
| **Hiki** ni **ki**wanda changu. | **Hivi** ni **vi**wanda vyetu. |
| **Hiki** ni **ki**faa changu. | **Hivi** ni **vi**faa vyetu. |

## Fundi hodari



Mjomba wangu ni fundi hodari sana. Alianza kazi yake punde tu alipotoka India. Yeye ana ujuzi wa kujenga nyumba, vibanda vya duka na hata viwanda. Pia mjomba huunda vitanda, meza hata na kabati. Katika ujenzi wake, yeye hutumia vifaa kama vile nyundo, misumeno, misumari, randa na gundi.

Tamka sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| w | sh | t | m |

Tamka silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| a | e | a | e |
| wa | we | wa | we |
| shwa | gwe | twa | mwe |

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: shwa ri - **shwari**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| shwa | nga | twa | i | ma |
| po | ha | nda | ri | we |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ini liko wapi? | Maini yako wapi? |
| Andazi liko wapi? | Maandazi yako wapi? |
| Dirisha liko wapi? | Madirisha yako wapi? |
| Pengo liko wapi? | Mapengo yako wapi? |

## Asubuhi



Asubuhi na mapema tuliitwa na mama. Anga ilikuwa shwari. Jua lilikuwa limechomoza. Mama akatwambia tuende kupatia kuku wishwa na kufungia mbwa. Tukamwambia mama kuwa hatujapata kiamshakinywa. Hapo ndipo mama alitupatia mkate mweupe. Kisha tukanywa chai kwa maharagwe. Tuliposhiba tukaelekea nje na kufanya kazi tuliyopewa na mama.

Soma sauti na silabi.

● b u ch u d u f u

**bu** **chu** **du** **fu**

Soma silabi na maneno.

▬ du ka ni su ka ri ma ja ni

**dukani** **sukari** **majani**

m ka te mi che zo cha i

**mkate** **michezo** **chai**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a li m tembelea a ka mu uliza

**alimtembelea** **akamuuliza**


ni li vyo ku tuma li li po tua

**nilivyokutuma** **lilipotua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Wakati uliopita** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Naitore **ali**mtembelea | Naitore **ata**mtembelea. |
| Babu **ali**muuliza | Babu **ata**muuliza. |
| Mama **ali**tuamsha | Mama **ata**tuamsha. |
| Omari **ali**ugua | Omari **ata**ugua. |



## Dukani

Siku moja, Naitore alimtembelea babu yake kijijini. Babu akamtuma Naitore dukani. Babu alitaka aletewe sukari, majani chai na mkate. Njiani, Naitore alikutana na marafiki wake. Walifurahi kuonana. Wakacheza michezo mbalimbali. Naitore akasahau kwenda dukani. Jua lilipotua, Naitore alirudi kwa babu. Babu akamuuliza, “Naitore, unatoka wapi? Wapi vitu nilivyokutuma?” Naitore alishtuka, “Oo, babu! Samahani. Nilicheza njiani hata nikasahau kufika dukani. Sitafanya hivyo tena”

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| s u | sh u | v i | f i |
| **su** | **shu** | **vi** | **fi** |

Tamka silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| su ru a li | wa si cha na | ma shu ja a |
| **suruali** | **wasichana** | **mashujaa** |
| so k si | b la u zi | s ke ti |
| **soksi** | **blauzi** | **sketi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu wa ambia | wana funzi |
| **huwaambia** | **wanafunzi** |
| i na itwa | ma shujaa |
| **inaitwa** | **mashujaa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mtoto **yuko** nje ya ofisi. | **Wa**toto **wako** nje ya ofisi. |
| Mdudu **yuko** chini ya meza. | **Wa**dudu **wako** chini ya meza. |
| Mgonjwa **yuko** juu ya kitanda. | **Wa**gonjwa **wako** juu ya vitanda. |
| Mwanafunzi **yuko** karibu na darasa. | **Wa**nafunzi **wako** karibu na madarasa. |



## Sare ya shule

Shule yetu inaitwa Mashujaa. Shule hii ina watoto wengi sana. Ina watoto wavulana na wasichana. Wao huvaa sare maridadi. Wasichana huvaa sketi nyekundu. Wanavaa pia blauzi ya samawati na soksi nyeupe. Wavulana huvaa suruali fupi. Wao pia huvaa soksi za kijivu na shati za samawati. Wanafunzi wote huvaa sweta za samawati na viatu vyeusi. Kila mara mwalimu mkuu hutuambia, "Someni kwa bidii."

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: du ka ni - **dukani**

★


| | | | |
|---|---|---|---|
| du | su | ka | ku |
| fi | ri | ki | shu |
| le | ni | si | ra |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| **Ni**nalala chini ya mti | **Tu**nalala chini ya miti. |
| **Ni**nacheza karibu na nyumba | **Tu**nacheza karibu na nyumba. |
| Ndege **yu**ko juu ya paa | Ndege **wa**ko juu ya mapaa. |
| Mpira **u**ko kando ya njia | Mipira **i**ko kando ya njia. |

## Rafiki Kalulu



Soma silabi na maneno.

ma wa i dha — **mawaidha**

ma a ru fu — **maarufu**

m jo mba — **mjomba**

vi ru si — **virusi**

kwa nza — **kwanza**

u ki mwi — **ukimwi**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ku ji kinga — **kujikinga**

wa si ambukizwe — **wasiambukizwe**

hu fundisha — **hufundisha**

a me ji funza — **amejifunza**

a na ishi — **anaishi**

hu saidia — **husaidia**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **ame**jifunza | **wame**jifunza |
| **ame**jikinga | **wame**jikinga |
| **ame**ishi | **wame**ishi |
| **ame**saidia | **wame**saidia |





## Hadithi ya Toili

Huyu ni Toili. Yuko katika darasa la kwanza. Toili anaishi na mjomba wake. Mjomba wake ni maarufu sana kijijini. Yeye husaidia wanakijiji kwa kuwapa mawaidha. Mawaidha haya huwasaidia kujikinga na virusi vya UKIMWI. Pia hufundisha watu jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI. Toili amejifunza mambo mengi kutoka kwa mjomba wake.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| vya ku la | tha ma ni | cha ku la |
| **vyakula** | **thamani** | **chakula** |
| mi ka te | mbo ga | ma tu nda |
| **mikate** | **mboga** | **matunda** |




Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u ta shangaa | na vi tamani |
| **utashangaa** | **navitamani** |
| hu ta kataa | vya tapakaa |
| **hutakataa** | **vyatapakaa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **-ako** | **-enu** |
|---|---|
| kalamu **yako** | kalamu **zenu** |
| kitabu **chako** | vitabu **vyenu** |
| mtoto **wako** | watoto **wenu** |
| jino **lako** | meno **yenu** |



## Lishe bora

Nina shairi jamani, ni fupi utashangaa
La vyakula vya thamani, ukipewa hutakataa
Vyote navitamani, naviona vyatapakaa
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

Lishe bora sio ghali, ni vyakula vya kawaida
Vya mikate na ugali, na mboga zenye faida
Matunda kwa kila hali, mafuta bila ziada
**Chakula sio utamu, sisitiza lishe bora**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: shu  ka - **shuka**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| du | le | ni | ku |
| su | ri | ra | shu |
| fi | ki | si | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| **Wakati uliopo** | **Wakati ujao** |
|---|---|
| Athumani **ana**kula | Athumani **ata**kula. |
| Omboga **ana**lia | Omboga **ata**lia. |
| Kalulu **ana**lala | Kalulu **ata**lala. |
| Toili **ana**ishi | Toili **ata**ishi. |

## Vyakula mbalimbali



Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| z i | s i | b a | p a |
| **zi** | **si** | **ba** | **pa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| zi wa ni | ku m la | ki to we o |
| **ziwani** | **kumla** | **kitoweo** |
| ba ku li | ba ta | kwe li |
| **bakuli** | **bata** | **kweli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku ku tembelea | a me nenepa |
| **kukutembelea** | **amenenepa** |
| a m tembelee | a ka mwa lika |
| **amtembelee** | **akamwalika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Bata **huyu** ni **m**zuri | Bata **hawa** ni **wa**zuri. |
| Dubu **huyu** ni **m**kali | Dubu **hawa** ni **wa**kali. |
| Kuku **huyu** ni **m**dogo | Kuku **hawa** ni **wa**dogo. |
| Nyoka **huyu** ni **m**refu | Nyoka **hawa** ni **wa**refu. |



## Dubu na Bata

Dubu alimuona bata barabarani. Akawaza, "Siku hizi bata amenenepa kuliko kuku!" Siku ya pili akakutana na bata ziwani. Dubu akamualika bata amtembelee. Lakini bata alielewa nia ya dubu ni kumla. Bata akasema, "Kwaa, kwaa, kwaa! Kukutembelea wewe ni kama kuweka kitoweo katika bakuli lako." Dubu akasema, "Kwa kweli, leo bata umenikataa. Siku moja nitakupata."

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| t e | v e | w e | y e |
| **te** | **ve** | **we** | **ye** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m bwa | ng'o mbe | nga mi a |
| **mbwa** | **ng'ombe** | **ngamia** |
| mbu zi | ngu ru we | si mba |
| **mbuzi** | **nguruwe** | **simba** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li shangazwa | wa li ishi |
| **walishangazwa** | **waliishi** |
| ha ku wapa | wa li kuja |
| **hakuwapa** | **walikuja** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Mimi** | **Yeye** |
|---|---|
| Ninapenda paka. | Anapenda paka. |
| Ninataka bata. | Anataka bata. |
| Ninapenda dubu. | Anapenda dubu. |
| Ninafuga mbuzi. | Anafuga mbuzi. |



## Siri ya Otonglo

Mzee Otonglo aliishi katika kijiji cha Mitimbili. Yeye alikuwa tajiri sana. Otonglo alikuwa maarufu kwa ufugaji wa wanyama. Katika zizi lake alifuga mbuzi, kondoo, na ngamia. Wanakijiji walishangazwa na Otonglo. Yeye alifuga fisi na simba pia. Wanyama hawa waliishi pamoja kwa amani. Watu walikuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Walikuja ili wajue siri yake. Otonglo hakuwapa siri hiyo.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: nga mi a - **ngamia**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| ka | ga | ta | nga |
| mbe | ng'o | pu | mi |
| nda | zi | mbu | a |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Wewe una**muona dubu | **Nyinyi mna**waona dubu. |
| **Wewe una**muona kuku | **Nyinyi mna**waona kuku. |
| **Wewe una**muona sungura | **Nyinyi mna**waona sungura. |
| **Wewe una**muona fisi | **Nyinyi mna**waona fisi. |

## Umoja wa siafu



Tamka sauti na silabi.

● a e

**wa** **we**

**nywa** **nywe**

Soma silabi na maneno.

▬ m si cha na | ku du mi sha | ku cha na

**msichana** | **kudumisha** | **kuchana**

m cha fu | nywe le | ku su gu a

**mchafu** | **nywele** | **kusugua**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ ha ku penda | ku m penda

**hakupenda** | **kumpenda**

wa ka m toroka | a ka furahi

**wakamtoroka** | **akafurahi**

Soma maneno haya.

◆

| **Neno** | **Kinyume** |
|---|---|
| safi | chafu |
| enda | rudi |
| juu | chini |
| kubwa | ndogo |
| lia | cheka |



## Msichana mchafu

Kando ya mto Mara, paliishi msichana aliyekuwa mchafu sana. Hakupenda kuoga, kusugua meno wala kuchana nywele zake. Kucha na nguo zake zilikuwa chafu sana. Siku moja, akaanza kujikuna kwa sababu ya chawa na uchafu. Wazazi wake, ndugu na marafiki wakamtoroka. Akabaki peke yake. Ndipo akaamua kuoga, kusugua meno, kuchana nywele na kukata kucha zake. Jamii na marafiki wakarudi na kumpenda tena. Msichana akafurahi sana na kuahidi kudumisha usafi.

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **i** | **a** | **a** |
| **wi** | **wi** | **wa** | **wa** |
| **kwi** | **mwi** | **chwa** | **mwa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u so ni | ki chwa ni | mwi sho we |
| **usoni** | **kichwani** | **mwishowe** |
| kwa pa ni | ma go ti ni | mi guu ni |
| **kwapani** | **magotini** | **miguuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa ka tu uma | tu me lala |
| **wakatuuma** | **tumelala** |
| wa ka toweka | tu li kuwa |
| **wakatoweka** | **tulikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | Kinyume |
|---|---|
| Savida **alichafua** rinda | Savida **alisafisha** rinda. |
| Mkoji **alianika** nguo | Mkoji **alianua** nguo. |
| Flora **alitega** mtego | Flora **alitegua** mtego. |
| Malenya **alipanga** vyombo | Malenya **alipangua** vyombo. |



## Siafu

Siku moja, siafu walikuja kwetu. Sote tulikuwa tumelala. Siafu wakatuuma kila mahali. Miili yetu ikafura. Walituuma usoni na kichwani. Pia wakatuuma mabegani, kwapani, mikononi na magotini. Mwishowe wakatuuma miguuni hata nyayoni. Jamii nzima ikalia kwa uchungu. Tulikuwa na maumivu kwa sababu ya kuumwa na siafu. Ilipofika asubuhi, siafu wote wakatoweka.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: si a fu - **siafu**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| m | si | cha | mu |
| ngu | fu | na | le |
| a | o | wa | te |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Nina**furahi sana | **Tuna**furahi sana. |
| **Nina**weza kusoma | **Tuna**weza kusoma. |
| **Nina**tafuta nyota | **Tuna**tafuta nyota. |

## Mafumbo ya maumbo



Tamka sauti na silabi.

| | |
|---|---|
| **u** | **i** |
| **vu** | **vi** |
| **mvu** | **mvi** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u pi nde | m vu a | nye ku ndu |
| **upinde** | **mvua** | **nyekundu** |
| ma chu ngwa | ma nja no | sa ma wa ti |
| **machungwa** | **manjano** | **samawati** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu ka unda | tu ka shindana |
| **tukaunda** | **tukashindana** |
| tu li po kuwa | ki ka shinda |
| **tulipokuwa** | **kikashinda** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Rangi **yangu** ni nyekundu | Rangi **zetu** ni nyekundu. |
| Sare **yangu** ni nyeupe | Sare **zetu** ni nyeupe. |
| Sketi **yangu** ni nyeusi | Sketi **zetu** ni nyeusi. |
| Kaptula **yangu** ni hudhurungi | Kaptula **zetu** ni hudhurungi. |



## Upinde wa mvua

Jana tulipokuwa shuleni kulinyesha mvua ya rasharasha. Mara tukaona upinde wa mvua angani. Upinde ulikuwa na rangi nzuri za kupendeza. Kwa kawaida, upinde wa mvua una rangi saba. Mimi na marafiki zangu tukashindana kutaja rangi za upinde wa mvua. Tukaunda makundi mawili. Ndipo tukataja rangi hizo kwa haraka. Kikundi changu kikataja rangi tano: nyekundu, machungwa, manjano, kijani kibichi, na samawati. Kikundi changu kikashinda.

Tamka sauti na silabi.

| ng u | ng a | ng o | ng e |
|---|---|---|---|
| **ngu** | **nga** | **ngo** | **nge** |

Soma silabi na maneno.


| be nde ra | hi s to ri a | nye u si |
|---|---|---|
| **bendera** | **historia** | **nyeusi** |
| u ku mbu sho | ma e nde le o | n chi |
| **ukumbusho** | **maendeleo** | **nchi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| hu tu kumbusha | tu ki pigania |
|---|---|
| **hutukumbusha** | **tukipigania** |
| i li yo mwagika | wa lio pigania |
| **iliyomwagika** | **waliopigania** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Rangi **hii** ni nyekundu | Rangi **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni nyeupe | Nguo **hizi** ni nyeupe. |
| Ngao **hii** ni nyeusi | Ngao **hizi** ni nyeusi. |
| Ngazi **hii** ni nyeusi | Ngazi **hizi** ni nyeusi. |



## Rangi za bendera yetu

Bendera yetu ni ukumbusho wa historia yetu. Rangi nyeusi kama ngozi yetu hutukumbusha mashujaa wetu waliopigania uhuru. Nyekundu hutukumbusha damu iliyomwagika wakati tukipigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi ni ukumbusho wa uzuri wa nchi yetu. Nyeupe ni ya amani. Amani ambayo hutufanya tuishi pamoja. Hii ndiyo nguvu, ngao, nguzo na ngazi ya maendeleo.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: nye u pe - **nyeupe**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| ja | ku | su | nja |
| ni | nye | si | no |
| ma | ndu | ki | pe |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| mkarimu | mchoyo |
| mzuri | mbaya |
| mrefu | mfupi |
| mkubwa | mdogo |
| mnene | mwembamba |

## Vitendawili

1. Nyumba yangu ni kubwa lakini mlango mdogo.
2. Mama nieleke.
3. Nawaka nateketea.
4. Tik tak tik tak.
5. Nikimpiga mwanangu watu hucheza.
6. Bubu mwenye maneno mengi.
7. Popote niendapo hunifuata.
8. Akija kila mtu analia.
9. Kipo lakini sikioni.
10. Wazungu wawili wamechungulia mlangoni.
11. Nyumba yangu haina taa.
12. Bak bandika bak bandua.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kifo | chupa | kitabu | ngoma | nyayo | kitanda | kivuli |
| mshumaa | kaburi | mate | saa | makamasi | kisogo | bunduki |

Tamka silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **i** | **a** | **i** |
| **ha** | **si** | **wa** | **pi** |
| **mha** | **msi** | **njwa** | **spi** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mu u gu zi | wa ki li | ma ju mba |
| **muuguzi** | **wakili** | **majumba** |
| m ha ndi si | mwa li mu | re di o ni |
| **mhandisi** | **mwalimu** | **redioni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu fundisha | a nge penda |
| **hufundisha** | **angependa** |
| hu hudumia | a tangaze |
| **huhudumia** | **atangaze** |


Sarufi: Soma sentensi hizi.

1. Kima yuko nyuma ya gari.



2. Mwalimu yuko mbele ya darasa.





## Jamaa ya Guyatu na kazi zao

Baba ya Guyatu ni mwalimu. Yeye hufundisha watoto wa shule ya msingi. Kaka yake ni muuguzi. Yeye huhudumia wagonjwa hospitalini. Mama yake ni mhandisi. Yeye hujenga barabara na majumba makubwa. Dada yake ni wakili. Yeye hutetea watu mahakamani. Guyatu angependa kuwa mwanahabari ili atangaze redioni na kwenye runinga. Wewe ungependa kuwa nini baada ya masomo yako?

Tamka sauti na silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **za** | **ja** | **wa** | **ta** |
| **nza** | **nja** | **kwa** | **kta** |

Tamka silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nje ma | kwa nza | u da k ta ri |
| **njema** | **kwanza** | **udaktari** |
| la zi ma | mwa shi | O g le |
| **lazima** | **mwashi** | **Ogle** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ni nge penda | ni ta saidia |
| **ningependa** | **nitasaidia** |
| ni fundishe | ni fanikiwe |
| **nifundishe** | **nifanikiwe** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Yule ni **mwa**namuziki | Wale ni **wa**namuziki. |
| Yule ni **mwa**nahabari | Wale ni **wa**nahabari. |
| Yule ni **mwa**shi | Wale ni **wa**ashi. |
| Yule ni **mwa**limu | Wale ni **wa**limu. |



## Kazi nizipendazo

Mimi ni Ogle. Niko katika darasa la kwanza. Nikimaliza masomo ningependa kufanya kazi mbalimbali. Ningependa kuwa mwalimu kama dada yangu ili nifundishe watoto kusoma. Mama yangu alisema ninaweza kuwa mwashi, nijenge majumba ya kifahari. Baba alisema udaktari pia ni kazi nzuri. Nitasaidia wagonjwa kupata nafuu. Ninajua kuwa ili nifanikiwe katika kazi yoyote ni lazima nisome kwa bidii.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: fu ndi - **fundi**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| ndi | to | mu | o |
| mwa | li | na | ndi |
| fu | nzi | shi | wa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Nina**enda sokoni | **Tuna**enda sokoni. |
| **Nina**enda barabarani | **Tuna**enda barabarani. |
| **Nina**enda nyumbani | **Tuna**enda nyumbani. |
| **Nina**enda shuleni | **Tuna**enda shuleni. |
| **Nina**enda dukani | **Tuna**enda dukani. |

## Mafumbo ya Wanyama

1. Kuku kumi waliangalia mwewe angani. Ni macho mangapi yalimuona mwewe? (Macho kumi, kuku huangalia juu kutumia jicho moja).
2. Kuna ndege kumi mtini. Ukirusha jiwe moja ni wangapi watabaki? (Wote watatoroka).
3. Mabaharia watano waliingia majini. Walipotoka, nywele zao hazikuwa na maji. Je, ni kwa sababu gani? (Mabaharia walikuwa na vipara).
4. Mwenye kuzaa hana miguu, mwenye kuzaliwa ana miguu. (Yai na vifaranga).

Soma silabi na maneno.

vi pe pe o
**vipepeo**

ku ngu ni
**kunguni**

pa nzi
**panzi**

chu ngu
**chungu**

m chwa
**mchwa**

nzi ge
**nzige**

Soma sehemu za neno na neno lote.

mbali mbali
**mbalimbali**

wa karibia
**wakaribia**

a li ye umba
**aliyeumba**

ku haribia
**kuharibia**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| wanene | wembamba |
| wakubwa | wadogo |
| kasi | polepole |
| ugumu | urahisi |
| uchungu | utamu |
| mwerevu | mjinga |



## Wadudu

Shairi nina kariri, la wadudu mbalimbali,
Wabaya nao wazuri, la nyuki wenye asali,
Vipepeo wa rangi nzuri, na chungu kila mahali,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**

Wengine wakaribia, kwa uchafu ulo ndani,
Mende na panzi pia, chawa nao kunguni,
Mchwa kuharibia, panzi na nzige shambani,
**Wadudu nao viumbe, ni Mungu aliyeumba.**


Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa du du | ka dhaa | ma fu pi |
| **wadudu** | **kadhaa** | **mafupi** |
| ma ba wa | hu fa ri ki | ma ya i |
| **mabawa** | **hufariki** | **mayai** |


Nyigu


Panzi


Mende



Nzi

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na pendeza | hu penda |
| **wanapendeza** | **hupenda** |
| hu patikana | hu fariki |
| **hupatikana** | **hufariki** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| -ake | -ao |
|---|---|
| Yai **lake** limevunjika | Mayai **yao** yamevunjika. |
| Nguo **yake** imeraruka | Nguo **zao** zimeraruka. |
| Mpira **wake** umepotea | Mipira **yao** imepotea. |
| Kioo **chake** kimepasuka | Vioo **vyao** vimepasuka. |



## Vipepeo

Vipepeo ni aina ya wadudu ambao wanapendeza sana. Hii ni kwa sababu ya rangi kwenye mabawa yao. Maisha ya wadudu hawa huwa ni mafupi sana. Wao huishi kwa wiki kadhaa tu. Kwa kawaida vipepeo wa kike hutaga mayai, halafu hufariki. Je wajua kwa nini vipepeo hupenda maua? Chakula cha kipepeo hupatikana kwenye maji ya maua.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: m bu - **mbu**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| wa | vi | pa | fu |
| pe | o | nzi | m |
| cha | ge | nza | bu |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|
| Kiwavi **ana**taga | Kiwavi **ata**taga. |
| Kipepeo **ana**vuka | Kipepeo **ata**vuka. |
| Siafu **ana**toroka | Siafu **ata**toroka. |
| Mende **ana**lala | Mende **ata**lala. |

## Hadithi ya Nzi



Soma silabi na maneno.

vi pa wa — ma ba di li ko — vyu ra

**vipawa** **mabadiliko** **vyura**

ku ta bi ri — ki a nga zi — m vu a

**kutabiri** **kiangazi** **mvua**

he wa — u pe po — jo to — hu hi si

**hewa** **upepo** **joto** **huhisi**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ hu ongezeka — u ta wa sikia


**huongezeka** **utawasikia**

ha wa onekani — wa ki imba

**hawaonekani** **wakiimba**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Yule | Wale |
|---|---|
| Mwalimu **yule** ni mzuri | Walimu **wale** ni wazuri. |
| Mwanafunzi **yule** ni mwerevu | Wanafunzi **wale** ni werevu. |
| Dereva **yule** ni hodari | Madereva **wale** ni hodari. |
| Mtoto **yule** ni mtiifu | Watoto **wale** ni watiifu. |



## Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya kwanza

Wanyama na wadudu wana vipawa vya kutabiri hali ya hewa. Wao huhisi mabadiliko ya hewa kama vile joto na upepo.

Vyura hawaonekani kwa urahisi wakati wa kiangazi. Wakati wa mvua, wadudu huwa wengi sana. Vyura nao huongezeka na kula wadudu hao. Ndio maana utawasikia vyura wakiimba kabla ya mvua kunyesha.

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| ba a dhi | ki wa ngo | ku twa |
| **baadhi** | **kiwango** | **kutwa** |
| u ta a la mu | m cha na | nzi ge |
| **utaalamu** | **mchana** | **nzige** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku tembelea | i me karibia |
| **kutembelea** | **imekaribia** |
| wa me ji ficha | wa me somea |
| **wamejificha** | **wamesomea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| mchana | usiku |
| baridi | joto |
| funga | fungua |
| nzito | nyepesi |
| rahisi | ngumu |
| vaa | vua |



## Utabiri wa hali ya hewa: Sehemu ya pili

Kwa kawaida, wadudu kama vile vipepeo hupenda kutembelea maua mchana kutwa. Mara tu unapoona wamejificha upande wa chini wa majani, mvua huwa imekaribia. Je, wajua kwamba nyenje nao huimba sana usiku.

Nchi yetu ina watu ambao wamesomea utaalamu wa kutabiri hali ya hewa. Wao wana ujuzi wa kupima kiwango cha mvua na joto. Wataalamu hawa huitwa watabiri wa hali ya hewa.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: u pe po - **upepo**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ju | vu | pe | u | to | wa |
| m | jo | a | po | pa | he |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mdudu **u**tamsikia | **Wa**dudu **m**tawasikia. |
| Mdudu **u**namsikia | **Wa**dudu **m**nawasikia. |
| Mdudu **u**limsikia | **Wa**dudu **m**liwasikia. |
| Mdudu **u**memsikia | **Wa**dudu **m**mewasikia. |

## Ndovu na Sungura



# Ndege na Wanyama

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m ku li ma | ngu ru we | ma zi wa |
| **mkulima** | **nguruwe** | **maziwa** |
| ng'o mbe | Na li a ka | a su bu hi |
| **ng'ombe** | **Naliaka** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li o nona | ku wa patia |
| **walionona** | **kuwapatia** |
| a li furahi | wa li endelea |
| **alifurahi** | **waliendelea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ng'ombe **ali**yenona | Ng'ombe **wali**onona. |
| Nguruwe **ali**yenona | Nguruwe **wali**onona. |
| Kuku **ali**yenona | Kuku **wali**onona. |
| Ng'ombe **ali**yekonda | Ng'ombe **wali**okonda. |



## Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya kwanza

Naliaka alikuwa mkulima hodari sana. Alifuga ng'ombe, kuku na nguruwe walionona sana. Kila asubuhi Naliaka alisema, "Kuku mweusi nitagie mayai ili nipate kiamshakinywa." Kila mara kuku mweusi alitaga mayai madogo na matamu. Ng'ombe naye alitoa maziwa ya kupikia chai. Naliaka alifurahi na kuwapatia kuku na ng'ombe chakula kingi zaidi. Wote waliendelea kukua vizuri.

Soma silabi na maneno.

gha la ni

**ghalani**

mwe u si

**mweusi**

so se ji

**soseji**

ni u a we

**niuawe**

m ku ta no

**mkutano**

dha ti

**dhati**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa li kuwa

**walikuwa**

ni me anza

**nimeanza**

a ka lalamika

**akalalamika**

a ka fikiria

**akafikiria**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mimi **nina**zeeka | Sisi **tuna**zeeka. |
| Mimi **nina**choka | Sisi **tuna**choka. |
| Mimi **nina**waza | Sisi **tuna**waza. |
| Mimi **nina**sema | Sisi **tuna**sema. |



## Mifugo ya Naliaka: Sehemu ya pili

Kuku mweusi na baba nguruwe walikuwa marafiki wa dhati. Siku moja wakawa na mkutano ghalani karibu na shimo la taka. Kuku mweusi akalalamika, "Mimi nimeanza kuzeeka. Nimechoka kutaga mayai kila siku. Mbona wewe hutoi hata angalau soseji moja kwa Naliaka?"

Baba Nguruwe akafikiria kisha akasema kwa huzuni, "Rafiki yangu, kwako wewe kutaga yai ni rahisi sana. Ili mimi nitoe soseji ni lazima niuawe."

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: chu ra - **chura**.

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| si | chu | ga | vu | ra |
| ndo | nya | ngu | ti | ku |
| twi | su | i | swa | mba |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Neno | Kinyume |
|---|---|
| haraka | polepole |
| ndani | nje |
| tajiri | masikini |
| juu | chini |

## Mfalme Simba na Sungura



# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

1

Kitabu hiki cha Kiswahili kimetayarishwa na kuchapishwa chini ya mradi wa TUSOME. Kimeandikwa kufuatia mwongozo wa mawanda na mfuatano uliofanyiwa utafiti wa hali ya juu kwa miaka mitatu katika mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini. Utafiti huu uliegemea kubuni njia mwafaka za kufunza usomaji na ufahamu.

Vipengele muhimu na vya kipekee kuhusu hiki kitabu ni:

- Kitabu hiki kinafuata mtaala wa taifa la Kenya.
- Mazoezi ya somo yamefuata mpangilio wa mantiki kutokana na utafiti wa njia bora za kufunza Kiswahili katika darasa la kwanza na la pili.
- Kitabu hiki kina michoro ya kupendeza ambayo hufanya somo la Kiswahili liwe la kuvutia.
- Masomo katika kitabu hiki hujumuisha vijenzi vyote vya lugha ambavyo ni; kusikiza, kuongea, kusoma na kuandika.
- Mpangilio wa kitabu hiki umekusudia kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa uzoefu kwa sababu kinawapatia nafasi ya kukumbana na vijenzi vyote vya kusoma.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

**Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.**

**Januari 2016**